

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**Verbatim Report of**

**DISSEMINATION OF REPORT & DRAFT BILL, ELDORET NORTH  
CONTITUENCY - T.A.C. (CENTRAL PRIMALRY SCHOOL)**

**ON**

**18<sup>TH</sup> OCTOBER, 2002**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL – ELDORET NORTH CONSTITUENCY HELD AT  
T.A.C. (CENTRAL PRIMARY SCHOOL ON 18<sup>TH</sup> OCTOBER 2002.**

**Present**

1. Salome W. Muigai - Commissioner

**Secretariat Staff in Attendance**

2. Gilbert Bor - District Coordinator
3. Dan Juma - Assistant Programme Officer
4. Asenath Kanga - Verbatim Recorder.

The meeting was called to order at **11.15 a.m.** with **Commissioner Salome Muigai** in the chair.

**Gilbert Bor (District Coordinator):** Kabla hatujaanza tuanze na maombi. Vile mnaona pale kwa ukuta umeelezwa kwamba uzime mobile kwa hivyo kama uko na mobile tafadhali uzime. Ukiangalia upande huu unaona imeandikwa silence ni kusema kwamba mkutano huu ni kama darasa. Naomba kwamba tuheshimu hiyo habari ya silence ili kila mtu aweze kusikika na kusikia kwa mkutano. Kurgat maombi.

**Mr. Kurgat: Prayer:** Kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu. Mungu Mwenyezi tunakushukuru kwa siku ya leo, tunakushukuru kwa wageni, tunakushukuru kwa wote ambao wamekuja kutoa maoni yao. Mungu mwenyezi utuongoze ili mambo yaende vizuri, yale mambo yote tutakayesema yatuwezeshe kuyapendi nchi hii kwa haki na amani. Tuanomba haya kwa jina la Yesu mkombozi wetu. Kwa jina la Baba, la Mwanza na la Roho Mtakatifu. Amen.

**Gilbert Bor:** Asante sana Bwana Kurgat. Commissioner nitachukua nafasi hii sasa ku-introduce members wa 3C's Eldoret North. Tafadhali msimame ili tuwajue. Hawa watu watatu ni Bwana Kurgat, Fatuma Sietenei kutoka upande wa Kidero, Bwana Paul Tanui kutoka upande wa Bartoi na Bwana Paul Kurgat kutoka upande wa Jua Kali. Wote ni watu kumi lakini wengine bado wanakuja. Asanteni.

Vile vile tuko na wale ambao walifanya Civic Education Eldoret hapa pia tunawakaribisha. Mjitambue wenyewe na mtujijulishe jina na kazi gani ulifanya.

**Robert Suiyot:** Commissioner na wote ambao wamekuja hapa, hamjambo. Kwa majina ni Robert Suiyot mimi ni Civic Educator katika Eldoret North upande wa Tarba, Muinde Location. Asanteni.

**Richard Kimtai:** Madam Commissioner, kwa majina naitwa Richard Kimtai nilikuwa mmoja wa Civic Educators, Eldoret North, Soi Division upande wa Loga Location.

**Mathayo Oranjo:** Madam Commissioner, jina langu ni Mathayo Oranjo, Civic Educator katika NCCCK.

**Juliana Nahumicha:** Naitwa Juliana Nahumicha kutoka Catholic Church.

**Gilbert Bor:** Haya, Asanteni sana. Kuna wengi ambao walihusika ambao wanakuja. Vile vile tuko na mmoja wa District Delegates ambaye anawakilisha Wilaya yet katika National Constitutional Conference tafadhali njoo ujitambue kwa watu ambao unaenda kuwakilisha.

**Emmy Kiprop:** Hamjambo, kwa majina naitwa Emmy Kipsoi Kiprop. Nilichaguliwa mama wa kuwakilisha kama District Delegate kuwakilisha akina mama na nafikiri nikisimama hata saa hii pia nitakuwa ninaakilisha vijana.

**Gilbert Bor:** Asante sana Emmy. Sasa Madam Commissioner ningependa kukupea nafasi kuanza mkutano wa leo na uendelee.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana Bor, wananchi wa kikao cha Bunge cha Eldoret Kaskasini. Hamjambo?

Nina furaha kubwa kwa niamba ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya na Mwenyekiti wangu Professor Yash Pal Ghai kwa ndio naona kuna wasome wengi nataka kutambua Mwenyekiti wangu, mtu mmoja wa wasomi, wakati yenye hayuko kwa hii habari ya kutengeneza Katiba yeye ni Mwalimu wa Chuo Kikuu Indonesia na anafundisha law. Na kwa niaba yake na niamba ya Wanatume wenzangu ningetaka kuwakaribisha kwenye kikao hiki.

Kwanza ningetaka kuwajulisha wenye tumekuja nao na pengine ningetaka kuwambia wajitambulisho ndio tusikia sauti yao.

**Dan Juma:** Majina yangu kamili ni Dan Juma. My work will be to take notes. Thank you.

**Asenath Kanga:** Hamjambo? Kwa majina naitwa Asenath Kanga na nitakuwa nina-recordi kila kitu yenye mtakuwa mnasena. Asenteni Sana.

**Com. Salome Muigai:** Asante na mimi mwenyewe naita Salome Wairimu Muigai na ninafuraha kubwa kuwakaribisha leo.

Kazi yetu ya Tume hasa ilikuwa kazi yenye ninaweza kugawanya kwenye njia tatu. Kazi yetu ya kwanza ilikuwa kuja kwa kila kikao cha Bunge na kuchukua maoni yenu na hiyo kazi tulifanya pamoja na wengine wenu. Halafu ilikuwa ni kazi yetu na jukumu yetu kuchukua haya habari yote tulipatiwa na tuitengeneza ikawa ripoti na kutengeneza reporti moja ndefu yenye volume tatu lakini bado hatujamaliza hiyo kabisa kabisa kuwa fair. Lakini tumetengeneza reporti fupi yenye kuleta maoni ya kila mtu yenye tulipatiwa kwa hii ingine na hiyo reporti ilikuwa kwa nakala za gazeti kama kwa Kiingereza tuliita “The Peoples Choice” pengine mliona kwa gazeti na ilikuwa pia kwa Kiswahili nakala inayoitwa “Chaguo la Wananchi”.

Tulikuwa pia na reporti kutekeleza mswada kwa kuomba kubadilishwa kwa Katibi, hiyo mswada yaani, Draft Bill ndio yenye tutayozungumzia leo na lengo la kuja leo kwangu ni ku-launch. Ku-launch ni kufanya nini?

**Speaker:** Kuzindua.

**Com. Salome Muigai:** Kuzindua. Haya, ndio Kiswahili hicho. Basi lengo letu leo ni kuzindua lakini kabla hatujazindua lazima tufikirie tutafanya nini. Tafadhali chukueni wenye mmefika na tuketi ili tuwe pamoja.

Nitangoja wenye wanakuja ili tuanze pamoja. Tafadhali ikiwa umeketi pahali kuna mwenzako mwenye analo na kuna mwingine mwenye hana wawili wape moja watumia pamoja. Kama kuna kiti bure ambacho hakijatumika tafadhali mpe mwenye hana kiti.

Wenye wamekuja nyuma mmekaribishwa kwa niaba ya Tume ya Merekebisho ya Katiba ya Kenya. Tulikuwa tumetambua majina yetu tukasema mimi ni Salome Wairimu Muigai na tumeandamana upande wangu wa kushoto na Bwana Juma kutoka kwa Tume ofisini ya Nairobi na pia tuna Bi. Asenath Kangu mwenye atakuwa aki-recordi mambo yenye tunazungumza moja kwa moja.

Ningetaka tukubaliane lugha gani tunaakikisha inatuwezesha kuwasiliana vilivyo. Mngetaka tuzingumze Kiswahili ama mngetaka tuzungumza..., kuna lugha tatu yenye tunaweza kuchagua. Kuna Kiswahili, kuna Kiiingereza na kuna .... Lugha gani yenye tutatumia? Kiingereza? Kuna mtu mmoja wetu mwenye haelewi Kiingereza hata kidogo kwenye hii chumba ama mwenye anaelewa tu Kiingereza? Haya, watu wangapi wangetaka tuzungumze Kiswahili, tafadhali inua mkoni kama ungetaka tuzungumze

Kiswahili na usiogope. Basi, kwa ajili wewe ungetaka tuzungumze Kiswahili tutazungumza Kiswahili. Kuna mtu mwenye

haelewi Kiswahili? Anybody who does not understand Kiswahili at all? Any Kenya who has been to school and does not understand Kiswahili? I thought Kiswahili was a compulsory subject in the 8-4-4. Anybody here who went to school before the mfumo wa 8-4-4? You do not understand Kiswahili at all? Are you a Kenyan? And you don't understand Kiswahili. The reason I am saying this is that a Kiswahili speaker might not understand English at all but all of us who are English speakers we understand some Kiswahili it is only that we will be better in English than we are in Kiswahili but we all who speak English also speak some kind of Swahili, it is the degree that differs. Whereas there is someone who understand Kiswahili and does not understand English at all so even if that person is just one, I would still want to use that language with your permission.

So can I revert back to our national language and speak Swahili?

**Audience:** Yes.

**Com. Salome Muigai:** Okay, some of the parts of course we will be mixing, it is very difficult to talk about a Constitution in just Kiswahili we might even try in some of the phrases need to look for our own mother tongue. Is there a mother tongue? Okay, we will look into that also, this is a time of reasoning together because we are making our Constitution and it is time to look at everything whether in mother tongue and researching whether there is a mother tongue and whether there is another tongue.

Kwa hivyo ningetaka kurudia kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili tena nisema kuwa ningetaka kufanya-introduction. Ni kufanya utangulizi tu kwenye hii Constitution. Hatuwezi kuisoma neno kwa neno. Tungetaka kuomba tafadhali mobiles zizimwe mostly because we are recording directly and we are going to interfere with our recording more than anything else.

Kazi yangu ni ya ku-introuce this document kwanza hatuwezi kuizungumzia neno kwa neno kwani ni document ndefu lakini nitawaomba tukishamaliza tupate nafasi ya watu kusoma.

Tafadhali huyo angeketi hapo na wewe uingie hapo nyumba at time it is difficult for some of us to go through between rows it becomes a major handicap rather than the availability of a disability. Thank you very much.

Kwa hivyo tutasema tunaanza, ningetaka kidogo kuwaeleza vile tulivyoona tulipoenda kuzungumzia wananchi juu ya urekebishaji wa Katiba. Kila pahali tulienda kulikuwa na mambo yenye kubadilisha Katiba lakini pia tulipoenda kama upande wa mipaka mwingine kulikuwa na mambo yenye ilikuwa ya muhimu kwa jamii moja kuliko vile ilivyokuwa muhimu kwa jamii nyingine. Kwa hivyo tutakapoendelea kuzungumzia hii Katiba nitaeleza kwa nini tulichukua chaguo moja badala ya mengine. Kila pahali yenye tulienda watu walikubaliana kuwa Katiba tulionayo sasa haina utangulizi yaani haina preamble na tukakubaliana kuwa yenye tutatengeneza hii mpya itakuwa na preamble. Kwa hivyo ukiangalia ukurasa wa pili, utapata kuna preamble ama utangulizi.

Preamble yetu kwanza inatutambua ni akina nani wenye kutengeneza Katiba hii na inasema ni nani?

**Audience:** We the people of Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Ni sisi wananchi ama watu wa Kenya. Pia inaendelea kusema, tukifahamu wingi wa tofauti zetu za nini? Tukifahamu wingi wa tofauti zetu za kikabila na nini tena.

**Audience:** Kitamaduni.

**Com. Salome Muigai:** Kitamaduni na kidini na kuijidhaminia kuishi kwa amani, kwa umoja kama taifa moja huru lisilofanya nini? Lisilogawika, tukijitolea kulea na kufanya nini? Na kulinda masilahi ya kila mmoja na ya nini nyingine?

**Audience:** Ya jamii.

**Com. Salome Muigai:** Ya jamii, ya jamaa. Familia ni nini? Ni jamaa ama ni jamii? Familia ni jamaa na community ni nini? Ni jamii?

Kwa hivyo tukijitolea kulea na kulinda masilahi ya kila mmoja, familia na jamii katika nini?

**Speaker:** Taifa letu.

**Com. Salome Muigai:** Katika taifa letu. Tukitambua matumaini ya nani?

**Audience:** Ya wanawake.

**Com. Salome Muigai:** Ya wanawake na nani? Na wanaume wetu, ya kuwa na serikali ambayo imejengwa katika musingi muhimu inayodhamini nini?

**Audience:** Uhuru.

**Com. Salome Muigai:** Uhuru na nini tena?

**Audience:** Democrasia.

**Com. Salome Muigai:** Democrasia na nini tena? Na haki ya kijamii na utawala wa sheria.

Tukitekeleza haki yetu isiyotengeka ya nini? Ya uhuru ili kutambua aina ya utawala wa nchi yetu na tukiwa tumeshiriki kikamilifu katika nini? Katika utaratibu wa kutengeneza ama kuunda katiba. Tunaifanya nini? Tunaikubali na tunafanya nini tena? Tunaifanya sheria na tunaitoa kwa nani?

**Audience:** Kwetu.

**Com. Salome Muigai:** Kwetu wenyewe na kwa nani mwingine?

**Audience:** Na vizazi vijavyo.

**Com. Salome Muigai:** Na vizazi vijavyo vya nani?

**Audience:** Vyetu.

**Com. Salome Muigai:** Vyetu na nini yenye tunatoa.

**Audience:** Katiba.

**Com. Salome Muigai:** Katiba hii. Na tonaomba Aibariki Mungu afanye nini? Alibariki Kenya. Kwa hivyo hii Katiba imetengenezwa na nani? Na sisi na tunaipa nani?

**Speaker:** Tunajipa wenyewe.

**Com. Salome Muigai:** Tunajipatia sisi wenyewe na tunawapa nani? Vizazi vijavyo. There are implications ya hiyo utangulizi kwa hivyo tafadhali tuchukulie vyema maanani kwani hiyo utanguliza utaeleza kila chenye tutaandika baada ya hivyo.

Kwa hivyo tukiangalia sura ya kwanza tunazungumzia uhuru wa wananchi na ukuu wa Katiba, tumesema kuwa wananchi, sovereignty of the people. Uhuru wa wananchi tunasema kuwa, mamlaka yote ya uhuru ni ya nani? Ni ya wananchi wa Kenya na yanaweza kutekelezwa tu kulingana na nini? Na katiba. Hio iko kwa katika ukurasa wa nne, uhuru wa wananchi.

Jambo la pili inaeleza kuwa wananchi watatekeleza uwezo wao wa uhuru kwa njia ya moja kwa moja, what does that mean? Directly. Au kupitia kwawakilishi wao watakaoteuliwa kwa njia gani? Ya democrasia. Kwa hivyo inaendelea pia kueleza habari ya uhuru wa wananchi. Halafu nambari ya pili inaeleza juu ya ukuu wa nini? Ukuu wa Katiba.

Ungetazama kwenye ukurasa ndio pahali yenye tutakuwa tukifanyia mazungumzo mengi lakini wakati mwingine tutakuwa kama wa bibilia, wale watu wenye hawajuhi kusoma Bible watakuwa na shida kusoma hii Katiba kwani tutakuwa tukiangalia hapa na kuenda kwenye vipengele tofauti kwenye, si Bible hata Quran imeandikwa kwa sura, sivyo? Kwa hivyo hii Katiba imeandikwa sura tutakuwa tukiangalia sehemu moja na nyingine.

Sura ile ya kwanza, jambo la pili ni ukuu ni wa Katiba na inasema hivi mwanzoni. Kenya imejengwa katika msingi ya ukuu wa Katiba na utawala wa sheria na itakuwa kwa mjibu wa Katiba. Who would like to read the first one in English, what does it say?

It says, Kenya is founded on the supremacy of the Constitution and the rule of law, it shall govern in accordance with what? With the Constitution so that is what we are saying in very many words in Kiswahili. I think this group would be more comfortable in English than Kiswahili but on the other hand I am afraid of leaving anybody behind. I am really afraid ya kumwacha yule aliyesema haelewi. Kwa hivyo, I will try my best to mix the two languages.

Hio sura ya kwanza inzungumzia uhuru wa wananchi, ukuu wa Katiba pia inazungumzia utekelezaji wa Katiba na hio ni nini kwa Kiingereza? Is what?

**Speaker:** The enforcement of the Constitution.

**Com. Salome Muigai:** The enforcement of the Constitution.

Number nne ni kufanya nini? Kulinda Katiba, Katiba ina haja ya kulindwa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Salome Muigai:** Kwa sababu?

**Speaker:** Watu wengine wanaweza kuiharibu.

**Com. Salome Muigai:** Inaweza kuharibiwa. Inaweza kuharibiwa kwa hivyo ina haja ya kulinda hiyo ni kweli kabisa.

Halafu nafasi ya tano inazungumzia juu ya sheria za Kenya, yaani sheria za Kenya zitatoka wapi? Sheria ya tano ya Kenya itatoka kwenye Katibia yenye tunazungumzia si hivyo? Pahali gani pengine tunatoa sheria? Wapi wasomi wa sheria hapa? La students, where do we get laws.



**Audience:** Parliament.

**Com. Salome Muigai:** Parliament, Bunge letu linaweza kuunda sheria zingine. Where else? Customary law inaweza kukubalika na pia wakati mwingine za kidini, si hivyo? Kama zile sheria za dini ya Kiislamu na pia common law, sheria za mazoezi zenye kila mtu anatumia. Kuna sheria zingine hazijaandikwa chini lakini pia sisi zote tunajua ni sheria. For example, ni shida sana kuvunja sheria yenye inasema usimtukane mtu, lakini ukimtukana mtu kila mtu anajua umefanya nini? Umefanya mambo mbaya. Kwa hivyo kuna hizi sheria zote zenye zitatumika kwenye hii jamhuri yetu.

Sura ya pili inazungumzia kuwa Kenya ni nini?

**Audience:** Republic.

**Com. Salome Muigai:** Republic ni nini?

**Audience:** Jamhuri.

**Com. Salome Muigai:** Ni jamhuri, na zungumzia kuwa Kenya itatangazwa kuwa jamhuri.

Nafasi ya pili yake, tutakubaliana...tafadhali kama kuna matatizo nieleze ili tuweze kuelewana zote. What is the problem? Because we are having another meeting down there and much as I would like to open the floor to my meeting. We need to come to a common understanding, what do you need to address? Is it the issue of language here? What is the problem? Ladies, I would like to hear your problems because you don't get many chances to be asked what our problems are. Kuna nini? We go on? Okay, that is okay.

Tunazungumzia habari ya jamhuri tuko kwa sura ya pili na nimesema kuwa swali la kwanza tunazumzia juu ya kutangaza Kenya kuwa jamhuri.

Ya pili inatuzungumzia juu ya eneo la Kenya. Nilizungumzia jamhuri lazima iwe kwenye map tunaweza kuonyeshana, this Jamhuri is within this boundaries. So that is the other point that I pointed on part seven, the territory.

Part eight inazungumzia mjii wetu mkuu na mji wetu au makao yetu makuu ni wapi? Ni Nairobi

Ya tisa inazungumzia lugha zetu rasmi na tunasema lugha zetu rasmi ni gani? Ni pili kuna nini na nini? Kuna Kiswahili na Kiingereza lakini pia tuna lugh ya taifa na hilo ni gani?

**Audience:** Kiswahili.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo kuna haja ya kutambua hivyo na kuweza kueleweka na kushauriana na kuwasiliana kwenye hiyo lugha.

Halafu ningetaka kumtambua Mwalimu wangu Bwana Bartulai uje wakati nakosa kuwa Commissioner nakuwa Mwanafunzi. Karibu sana Mwalimu, Bwana Bartulai amenifundisha kwenye Standard Five katika Township School, kwa hivyo Kiingereza kile kizuri na Kiswahili ni chake na kile kibaya ni changu. (*Laughter*) Karibu sana Mwalimu.

Tunazungimzia habari ya lugha kwani tuko kwenye sura ya pili ya maandishi yetu na tunaangalia lugha zetu na tunasema kuwa tuna lugha mbili rasmi, Kiswahili na Kiingereza lakini pia tuna lugha ya Kiswahili yenye tunaweka maanani kama lugha ya taifa. Nitabaini pia tumetambua lugha ya Ishara, tumesema sign language itakuwa pia lugha ya kuweza kufundishwa na kueleweka kwani pia itakuwa lugha yenye inatumika Bunge, kuwa lugha za kirasmi ya Bunge zitakuwa tatu, Kiswahili, Kiingereza na lugha ya Ishara, kwa ajili ya wenzetu wenye hawatunii masikio kusikia lakini wanatumia macho yao.

Tumesema pia kwa maandishi yetu ingawa tutaandika kwa maandishi rasmi kwa Kiswahili na Kiingereza, tutajaribu sana mara nyingi nyingi kuandika kwa lugha ya Braille pia ili kuwahuzisha wenzetu wenye hawaoni kwani hii Katiba mpya yawalete waKenya wote kuwa Jamhuri na taifa ngapi?

**Audience:** Moja.

**Com. Salome Muigai:** Tumezungimzia pia habari ya taifa na dini na tumesema kuwa Kenya sio taifa la kidini lakini ni taifa linalotambua dini na kila dini itapatiwa usawa moja na nyingine na pia watu wengine wanatuuliza, kama tuna usawa moja kwa nini dini ya Kiislamu imepatia koti zake, mahakama yake lakini sio za Kiikriso. Naeleza kuwa wa historia watatueleza zaidi lakini wakati tulipokuwa tunakubaliana habari ya uhuru wetu mnakumbuka kuwa kwenye Mkoa wa Pwani kulikuwa nafasi moja ya maili ngapi? Kumi yenye ilikuwa sio pamoja na Kenya, ilikuwa na mali ya nini?

**Audience:** Sultan.

**Com. Salome Muigai:** Sultan wa wapi?

**Audience:** Wa Zanzibar.

**Com. Salome Muigai:** Wa Zanzibar kwa hivyo makubaliano ya Kenya na Sultan ili tupate hicho kitengo hicho kuwa ni

pamoja na Kenya ilikuwa kuwa Waislamu watakubalishwa mahakama yenye itafanya sheria za kibifasi yaani, personal law inayohusu kuoa, kuolewa, talaka, urithi, kufa, kuzikwa, vitu kama hivyo. Sasa hiyo ndio contract of that agreement, we are still honouring that because it was a commitment. Sasa sio habari ya kidini tena, ni makubaliano yenye tulifanya ndio Kenya ikuwe nchi moja. Wakati mwingine tukitaka kufanya watu wawe pamoja, there is a cost and unless you have to decide whether the cost is enough for what you are getting back and I think there was one time when there was an agreement to create a united Kenya that was to be agreed upon.

Halafu tuna alama za taifa, alama zetu za taifa ni kama nini?

**Audience:** Bendera.

**Com. Salome Muigai:** Bendera yetu. Nini tena?

**Audience:** Wimbo wa taifa.

**Com. Salome Muigai:** Wimbo wa taifa. Wangapi wanajua wimbo wa taifa? Kwa Kiswahili ama kwa Kiingereza? Yote, okay that is good. Walikuwa wawili, wangapi wanajua wimbo wa taifa? Mnajua mimi ni mwalimu huenda nikauliza kila mtu asimame hapa aimbe lakini ni vibaya leo Mwalimu wangu ameingia. Unajua hata ukiwa na miaka ngapi, mwalimu wako akiingia unasikia umekuwa mwanafunzi kidogo. Kwa hivyo kwa ajili ya Mwalimu wangu sitawauliza muimbe huo wimbo lakini hiyo ni moja ya ishara zetu za kutueleza sisi kama nini? Kama taifa na nini? Na Jamhuri.

Tumezungumzia lugha la taifa na bendera na nini tena?

**Audience:** Court of arms.

**Com. Salome Muigai:** Si, sikii, hiyo ni nini? Koti ya mkono? (*Laughter*) Court of Arms nimeambiwa na wasomi wenye kujua Kiswahili hua inaitwa nembo. Halafu nini tena, ishara nyingine ni nini?

**Audience:** Muhuri.

**Com. Salome Muigai:** Ni muhuri wa nini? Muhuri wa taifa. Halafu pia kwenye hi Katiba mpya tumesema wale wenye watakaowapatia wadhifa wa kutuongaza tutawapa kiapo ama nini? Matamko ya dhati.

Halafu mwishowe tumezungumzia habari ya siku za taifa. Mmekuwa na maswali mengi kwa hivyo nitayajibu kabla sijaulizwa. Kuwa tumeona mmeondoa Kenyatta Day, mmeondoa Moi Dai mmebakisha tu siku ya Madaraka na shikuku ya Jamhuri na pia

tumependekeza siku ya Katiba. Kwa nini mlifanya hivyo? Kuna watu wengi walitoa maoni kuwa hizo siku ziondolewe zenye majina ya watu lakini hata zaidi ya hayo kwenye Katiba iliyoko sasa hata kabla hatujaguza hii mpya, tumesema kuwa tutakuwa na Rais kwa miaka mingapi mwisho?

**Audience:** Kumi.

**Com. Salome Muigai:** Miaka kumi yaani mihula miwili ya miaka tano kila mmoja, kwa hivyo ni miaka kumi. Kwa hivyo katika usoni, miaka mingine hamsini zijazo na wengi wetu kama hatutakufa kwa ajala huenda tukawa bado tuko hai, inshalla. Miaka mengine hamsini hijayo tutakuwa tumepata Rais wangapi at least?

**Audience:** Watano.

**Com. Salome Muigai:** Watano ama moja ama mwingine asiporudishwa mara ya pili tunaweza kuwa na Rais kutoka watano mpaka kumi. Sasa tukiwapa kila mtu siku yake itakuwa shida, sijui tutafanya uchaguzi aje kusema Salome akiwa Rais tutampa siku lakini Nahumicha akiwa Rais hatumpi siku yake ndio kwani tulisema kuwa kwanza fikiria hali isiyolingana na mtu yenye inaweza kuweka siku zetu za taifa, kama siku ya Madaraka, itabaki siku ya Madaraka miaka yote, si hivyo? Siku ya Jamhuri itabaki hivyo. Tukianzisha Katiba mpya, siku ya Katiba itabaki siku ya Katiba. Sasa nitataka maoni yenu lakini nilikuwa nafikiri ni vizuri kufafanua pale.

Tukienda kwa sura ya tatu, inaeleza nini?

**Audience:** Malengo.

**Com. Salome Muigai:** Inaeleza malengo ya taifa na nini? Maadili na kanuni. Malengo, maadili na kanuni. Hayo malengo yanaonyesha dhamana zetu, our values na ningetaka kusoma machache tu kwani ni mengi.

Ningetaka kuanza na malengo ya taifa, ni nambari ya kwanza. Malengo ya taifa, maadili na kanuni zilizomo katika sura hii zinahusu mamlaka ya nchi yaani, the Executive, Bunge yaani Parliament, Mahakama, nini hiyo?

**Audience:** Judiciary.

**Com. Salome Muigai:** Judiciary, tawala za Wilaya na vyombo vingine vya serikali na viongozi, raia, miungani ya kibinafsi pahali ambapo chombo kimoja kinatumia na kuifafanua katiba au sheria nyingineo, hiyo ni (a). (b) kinatumia, kinaunda na kutekeleza maamuzi ya nini? Policy? Sera. Neno sera linatoka kwa siasa kama vile neno policy linatoka kwa nini? Kwa politics. Naona watu wanashida na kiswahili kabisa.

These are our values, I would like to explain this because it is very very important that these are our values, they are our? As well as values they are what? It is written there, my good teacher who allowed me to present the draft you are looking at the table. We have gone back to Kiswahili so read it. Stop looking so out of the whole thing, now we are in English mode. So we are looking at our what? We are looking at our goals, our values and our principles.

So let us look at the three of them and we are saying that these goals and principles apply to who of what? They apply to the executive, to the Legislature, to the Judiciary and even to the District Governance as well as what?

**Speaker:** All of us.

**Com. Salome Muigai:** Exactly. That if we are going to amend all of us in our implementation of whatever constitutional value we agree on. So lets look at them and see what they are.

Ya kwanza ni kuwa jamhuri itaguza umoja wa taifa na kuendeleza hali ya kujitolea kwa raia wake kwa mwito wa nini? Wa taifa. What is that in English?

It says, the republic shall promote national unity and develop the commitment of its what? It citizens to the spirit of nation unity. (iii). The republic shall recognise the diversity of its people and promote culture in its communities.

So we are going to recognised this because in our preamble we said that we are aware of our diversity in culture then we are going to make sure that we nature this diversity. However, look at what we had first, is the fact that while naturing this different diversities we are going to remain what? A nation and we are going to remain united or divided? We are going to remain united.

Then it says that the republic shall ensure open and transparent government and the accountability of what? State officials and public authorities and so on and so on. There are many values that we expounding in this chapter.

But I would like to read number...ningetaka kusoma kipande cha kumi na moja before I finish with them. Ningetaka kusoma kipengela cha kumi na moja, asante sana na inasema hivi. Nitasoma kwa Kiingereza. The republic shall ensure the fullest participation of who?

**Audience:** Women.

**Com. Salome Muigai:** The women and who else?

**Audience:** The disabled.

**Com. Salome Muigai:** The disabled and the marginalized communities and the rest of the society in the political, social and economic life of the country. Those are our principles, those are our values and those are our what?

**Speaker:** Our goals

**Com. Salome Muigai:** Our goals. The following one ama ya pili inasema, Serikali itatekeleza kanuni kuwa theluthi moja ya wanachama wa vyombo vyote vinavyofanyiwa uchaguzi na uteuzi ni nini?

**Audience:** Ni wanawake.

**Com. Salome Muigai:** Ni wanawake. Number four says, the State shall and you know when you say shall, what do you mean?

**Audience:** ...must

**Com. Salome Muigai:** Sio choice wakati inakupendekeza unahaja na saa ile haipendezi unafanya nini? Unawacha. Hii inasema the State shall impliment the principle that one third of the members of all elective and appointive bodies shall be women.

Ningetaka pia kuzungumzia, kipengele cha kumi na tatu chenye kinasema hivi. The republic shall recognize the special responsibilities that the State, society and parents owe to our children and shall ensure their material and moral wellbeing. Those are three of the values that I am looking into but nitaomba msome hiyo sura mpaka mwisho ndio tuelewe zingine zenye mmefikiria.

Pia kwenye hiyo sura tuna wajibu wa wa raia and that is what? Duties of a citizen, what are the duties of a citizen, they have been numerated there. Imeelezwa kwa kinaganaga ili tuelewe vilivyo. Sitawasomea wajibu kwani wajibu usipousoma na usipoujua, ignorance is not a defence, kwa hivyo kila mtu anasoma wajibu wake. Ningetake tuangalie sura ya nne.

Sura ye nne inazungumzia uraia, inazungumzia habari ya kanuni za jumla kuhusu uraia, pia inazungumzia kudumisha uraia uliopo, kama wewe ni raia tayara unahitaji kufanya nini ndio udumishe nini? Uraia wako or how to retain your citizenship. Then it talks about, kupata uraia kama tayari huna na inazungumzia pia juu ya uraia wa kuzaliwa na uraia wa nini tena? Uraia wa kuo na kuolewa (ndoa), Kisha inazungumzia pia habari ya watoto wanaopatikana Kenya na watoto wachanga. Hii maana yake ni

kuwa, mtoto yoyote akipatikana Kenya, akionekana kama ana miaka nane, kwa nini tunasema akiwa na miaka nane? Tunasema akionekana kama ana, seemingly eight. Kwa nini tunatumia hiyo neno, sio kusema akiwa miaka nane? Kwani akiwa anapatitakana na hajulikani wazazi, hajulikani ni nani, atajijua yeye mwenyewe ana miaka ngapi? La, kwa hivyo mtoto akionekana ana miaka nane na hajulikani alikotoka ama hatumwelewi pahali anaenda, tutamfanya awe Mkenya, atapata uraia. Watu wengi wanatuuliza, miaka nane ina maana gani? Nasema, kuna kipengele kingine chenye tutasema kuwa elimu itakuwa ya lazima na ya bure, kwa hivyo mtoto wa miaka nane bado tunaweza kumweka kwenye shule.

Kwa hivyo mtoto wa miaka nane bado tunaweza kumweka kwenye nini? Kwenye shule. Kwa hivyo mtoto wa miaka nane mwenye anaweza kuenda shule tutamtambua kuwa Mkenya. Akiwa na miaka kumi na tano basi atatueleza yeye ni nani na alitoka wapi? In the English version watu walikuwa wameita founding lakini tukasema hiyo ni lugha, a founding language is laboratory language na kwa hii Katiba kuna pahali pengine tunaona tumekataa kabisa lugha yenye kuleta sifa ya mtu yeyote chini. Iwe sifa ya kuleta mtu aliyena ulemavu chini, imekataliwa na Katiba. Iwe ni sifa ya kuleta akina mama chini, imekataliwa ndani ya Katiba. Hasa utamaduni wetu tunasema, tunaukubali tu mwenye haugagui mtu yoyote, wenye kubagua mtu yeyote, utakuwa umegeuka nini? Katiba na tunasema Katiba ndio sheria ile iliyokuu. Kwa hivyo yote yenye kugeuka Katiba haiwezekani kutekelezwa.

Tumezungumzia hii neno kwenye Kiswahili inaandikwa uraia maradufu ingawa mimi sio msomi wa Kiswahili. Hatukusema tunataka raia maradufu, tulisema tunataka raia wa nchi mbili, maradufu ni multiple. That is it. Vile tunasema ni dual citizenship. Hiyo watu wengi wametuuliza kwa nini mliweka hiyo. Tulipoenda kwenye jamii zetu wenye wakukaa mpakani tuliambiwa kuwa wanahitaji kuenda na kurudi kwenye nchi zile zingine ndi waweze kujisitiri. Kama jamii zetu za Kimaasai walisema, wakati wa kiangazi wanavuka kuenda nchi ya jirani ya Tanzania ili mifugo yao ifanye nini? Isife, kwa hivyo wanataka kuwa sisi tukiwa Wakenya tusiende Tanzania tutakuwa tumeua uchumu wao na maisha yao. Kwa hivyo, hiyo ilikuwa jamii moja ya Kimaasai. Jamii zingine zipi zenye kukaa mpakani kwenye kuwa kwa nchi mbili? Which other communities live along our boundaries?

**Audience:** Somali.

**Com. Salome Muigai:** The Somali, they had the same argument that during drought season, they have to cross borders to go to the other places to nature and nourish their livestock and then come back when things are better. Any other communities?

**Audience:** The Sebeyi.

**Com. Salome Muigai:** The Sebeyi, Pokot, Teso, Samia, Luo, Turkana, Kuria, Bukusu. Eh, Nahumicha why are aren't you leaving us when there is famine is on this side we cross the boundary. So those are the communities, hii ilikuwa concern ya jamii zenye kuishi huko, kwa hivyo tumesema hii Katiba mpya inakubalisha Mwanakenya kuwa raia wa nchi yetu na raia wa nchi

nyingine mradi tu asiwe raia wa nchi isiyo rafiki ya Kenya.

Pia tumezungumzia habari ya kuanzishwa uraia, tumezungumzia habari ya uraia wa uzazi kabla mtu hajazaliwa. Kama baba amekufa kama mtoto hajazaliwa, huyo mtoto atapatiwa uraia yenye angepatiwa kama wazazi wake wote wangukuwa hai. Tumezungumzia pia makao kwa ajili wanaweza kukaa na uwezo wa Bunge juu ya uraia na pia tumaanzisha almashauri ya kusajili uraia. Kwenye Katiba yetu iliyoko sasa, mwanamme akimwoa bibi mgeni anaweza kumridhisha bibi yake uraia lakini mwanamke Mkenya akiolewa na mtu asiye Mkenya hawezi kumridhisha bwana wake uraia wala watoto wake na hii kwani nilisema tutaendelea kwa sura hiyo ingine inasema, una uhuru kutoka kubaguliwa kwa maana tuliona kama hapo kuna kubaguliwa. Kwa hivyo tumetoa na kusema mtu yoyote anayezaliwa na mzazi mmoja akiwa Mkenya, huyo mtoto anahaki ya kuwa Mkenya na Mkenya yoyote akioa ama akiolewa anaweza kumridhisha mumewe ama mukewe uraia wa Kenya baada ya miaka tatu.

Sura ya tano inazungumzia sheria za haki. Tumesema habari ya haki za kimsingi na uhuru, tumezungumzia ni wajibu wa serikali kuendeleza haki na uhuru, tumezungumzia habari ya mipaka ya haki, yaani hakuna haki yenye haina nini? Kikomo, kila haki inakikomo chake. Kwa mfano, unaweza kuwa na haki ya kutembea na kuenda pahali popote utakapo lakini ukivunja hiyo sheria yenye kukupa hiyo haki nayo sheria inatatiza hizo haki zako.

Tunazungumzia pia habari ya haki ya kuishi, the right to life na kwa ajili ya haki ya uai yenye hakuna mtu mwenye kumpatia mwingine. Watu wengi sana walituomba tuondoe adhabu ya kifo na hii Katiba imeondoa adhabu ya kifo, ama imependekeza. Haya mambo yote ni mapendekezo tuelewane ndio bado tunaita draft. Na hii draft itaenda kuzungumzia na wale delegates wenye tumeona hapa. Nitaeleza kidogo juu ya hiyo.

Tumezungumzia haki ya usawa, equality before the law na ningetaka kueleza kidogo hapa. When we say that we are equal, we don't mean we are the same. There is a major difference between being equal and being the same. When I say that a Kalenjin and a Luo are equal, do I mean they are the same? No. Do they have the same language, do they eat the same food, do they have the same culture? But are they equal? Yes. So when we say that men and women are equal also we don't mean they are the same, we just mean that each has the same rights. If one has a right to life, the other one has a right to life na hizi haki zote zenye zimetajwa hapa.

The right to equality, right to all manner of things. Kila mtu ana hizo haki lakini hatusemi watu wamekuwa the-same. Tukisema watu wenye ulemavu are equal to people without disability, are we saying they are the same? No, if you have two children and one has a disability and the other one has no disability and we say they don't have equal rights to education, what do we mean? We mean that we are going to give them both education and we are going to put that extra that is needed for the child with a disability to ensure that they also have to access equality in education. So we are saying, its only after we have respected the



right to equality that we look at equity. Because that child with a disability will need some special intervention and that is equity now, giving them what they need in order to get what they equally deserve. Do you understand me? Because these are principles we have got to understand well otherwise it worries us, there is a concern. How can we say people are equal, does that mean that they are the same?

You hear people many times say that, kwa sasa vile akina mama na akina baba tumetoshana hakuna haja ya kumfungulia mlango ya gari, no. Hukunifungulia kwa hivyo hatukutoshana, ulinivunguliwa kwani, although we are equal we are not the same.

That is why we have different roles. So there is a right to equality and you can read what the provision says.

Then we have the freedom from what? From discrimination on whatever level, you should not be discriminated against because you are what? can you read such provisions. The State shall not unfairly discriminate directly or indirectly against anyone on any unworthy grounds including race, sex, pregnancy, marital status, ethnic or social origins, colour, age na zingine nyingi zenye hakiko kwenye kwenye hiyo utaratibu. No discrimination on any ground, so you have freedom from discrimination.

Kuna haki za makundi tofauti yenye imeadhirika hapo mbeleni, kwa hivyo hii Katiba mpya inaoneshana haki za wanawake. Pia kuna hazi za wazee katika jamii. Tumesema ni wajibu wa mzee akiwa kijana ajiwekee mali yake na ajiangalie mwenyewe akishakuwa mzee. Lakini asipoweza kufanya hivi ni wajibu wa taifa kuwatazama wazee wetu na ahadi zingine zilizonyingi. Wakati mwingine wazee sana hekima zao zimetolewa ndio tunawaondosha katika hali ya kuishi, si hivyo? Na kwa sasa lazima kwa hii Katiba mpya tuwatafutie nafasi yao ya kushiriki kwenye maisha ya kila siku.

Tuna haki za jamii na tuna haki za watoto, tuna haki za familia na tuna haki za walemavu ama watu wasiojiweza lakini watu hawapendi ilo matamko hata kidogo, ati wasiojiweza. Wangetaka kuitwa watu wenye ulemavu, kwani ni mtu kwanza halafu ulemavu unakuwa wa pili.

Pia tumezungumzia habari ya heshima za binadamu yaani. Heshima za binadamu ni nini?

**Audience:** Human dignity.

**Com. Salome Muigai:** Human dignity. Tumezungumzia pia uhuru na usalama wa mtu, tumezungumzia uhuru wa kutofanywa mtumwa ama kufanywa nini? Ama kufanywa sulubu ama topoa. You should not be made into a slave, you should not be forced to work without pay and you should not be forced to labour. Kuna right to privacy, kabla mtu hajaingia nyumba yako atachukua masharti yenye Katiba imeweka ili wewe uwe na haki ya faraga.

Kuna uhuru wa dini, imani na maoni, kuna uhuru wa kutoa maoni, kuna uhuru wa kuyachapisha hayo maoni sharti moja tu usiwe maoni yako ni ya kutatiza jamii, ni ya kuleta chuki ama ni ya kuleta kutoelewana kati ya jamii moja na nyingine ama kati ya mtu

moja na mwingine.

Kuna uhuru wa kushirikiana, kuna uhuru wa kufanya mkutano, maandamano, kuchochea mgomo na una uhuru wa malalamiko, inaweza kuwa malalamiko yako. Kuna uhuru wa haki za kisiasa. Uhuru wa kuenda utakako na kufanya nini? na kuishi au kukaa huko. Kuna uhuru wa wakimbizi na pia kuna uhuru wa bishara na kazi za nini? Za ujizi.

Kuna uhuru wa kuwa na mali, uhusiano wa kikazi, usalama wa kijamii na uhuru wa afya na nini tena?

**Audience:** Elimu.

**Com. Salome Muigai:** Elimu, nyumba ama makao, chakula, maji safi, usafi na nini tena? Na mazingira. Jambo mpya kuhusu mazingira nilisema kila mmoja kwenye Katiba hii ataweza kuenda mahakamani kusema mazingira yeke inaharibiwa. Kila mtu ana uhuru wa kuenda mahakamani kuyalinda mazingira yake kwa ajili yetu na kwa ajili ya nani mwengine?

**Audience:** Vizazi vijazo.

**Com. Salome Muigai:** Kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Kuna uhuru wa lugha za kitamaduni, unaweza kuzungumza lugha yako ya kitamaduni lakini uhuru wako unaishia wapi? Uhuru wako unaishia pahali uhuru wa mwenzako inapoanza. Yaani nikisema nina uhuru wa kuzungumza lugha ya baba na ni kweli nina uhuru, nianze kuzungumza lugha hiyo na mimi nazungumzia mambo ya public na wengine hawaelewi, sasa uhuru wangu umepita mipaka ya nini? Ya watu wele wengine, si hivyo? Kwa hivyo uhuru wangu unakomea pale uhuru wako utafanya nini? Unaaanzia.

Kuna uhuru wa haki za wateja, utawala wa haki, haki ya kutofuata maagizo yasio halali. Hiyo ina maan gani? Hiyo mara nyingi sasa imeletwa kutokana na janga lililolipata Rwanda na makabila zingine na Ugoslavia. Pahali watu wameuwa wakiulizwa wakiletwa mahakamani wanasema kuwa walikuwa wanafuata nini? Walikuwa wanafuata amri. Sasa wameambiwa huwezi kufuata amri ikiwa hiyo amri isiyo halali na ukifuata hutajitetea kwa kusema ulikuwa ukifuata amri.

Kuna uhuru wa kufikia mahakama na kuna haki ya watu wanaotiwa nguvuni. Watu wengi walitueleza kwamba unaweza kutiwa nguvuni utakaa wiki mbili kabla hujaletwa kwenye mahamakama na hujaachiliwa. Kwa hivyo sasa tumeweka masaa fulani ndio mtu anatakiwa kukaa kwenye mahakama na ikizidi hiyo lazima aachiliwe.

Pia kuna uhuru wa kufanyiwa mashtaka ya haki na ya muda. You have a right to a fair trial but timely trial also. If you are going to get a fair trial after 5 years of remand then can that be fair? No, so we are talking about time frame here as part of the

fairness of the trial.

Kuna pia haki ya watu waliokizuizini na pia wakati wa hatari haki zetu zingine zinaondolewa kwa muda, si hivyo? Unasikia kuna curfew lazima uwe nyumbani saa ngapi na time, si hivyo? Lazima ufanye jambo moja au lingine. Kwa hivyo wakati wa hatari t.

...umeandalia kwa kirefu ili tuone utafanyika vipi na utafupishwa vipi ili watu wawe na haki na uhuru wao. Pia matumizi ya sheria yetu ya haki na tumeunda kikundi ama Tume ya kuangalia haki zako na utawala venye unataka. There will be a place where you can take your complaints when you feel that your rights and your freedom have been abused, misused or used against you.

Tumeuliza mahakama kuwa na mamlaka ya kulinda hizi haki. You can go to court also kusema haki zako zimefanywa nini? Zimekeukwa

Kuna jambo moja ningetaka kusema kabla hatujaondoka kwenye hiyo sura na tutakubaliana vile tutafanya mtu mwingine mwenye itafanya Katiba yetu ya mkutano huu. Mtu mwenye ataendelea kutatiza recording zetu kwa kuwa na mobile tutamfanya nini? Haki zake gani zenye tutampokonya kwani hafuati sheria zetu.

**Audience:** Ataenda nje.

**Com. Salome Muigai:** Ataenda nje ama tutachukua mobile, tufanya nini nayo? Tumpatie mwenye hana. (*Laughter*).

Kuna jambo moja yenye ningetaka kutazama kwa upangilio wa sura. Mnaona sura ya haki ni sura ya ngapi?

**Audience:** Ya tano.

**Com. Salome Muigai:** Ya tano na kwa pahali ya wajibu wa raia ni sura ya ngapi? Duties of the citizen are on which chapter?

**Audience:** Chapter four.

**Com. Salome Muigai:** Chapter four, so what are we saying about rights and responsibilities, which one comes first according to this, mpangilio wenye uko hapa. Lipi linakuja kwanza?

**Audience:** Kazi kwanza.

**Com. Salome Muigai:** Yes, our duties come before our rights. Yes because we don't do what is right, you don't have to

enjoy our rights. So we have deliberately on this document put the duties before the rights.

Basi sasa sura hizo za kwanza tano zenye tulikuwa tunataka tuangalie kwa urefu hizi zingine tutapitia kwa ufupi zaidi kwani hii Katiba in sura ishirini na sasa tuko kwa sura ya ngapi? Ya tano, bado tuna ngapi zimebaki?

**Audience:** Kumi na tano.

**Com. Salome Muigai:** Kumi na tano na zingine tuna vipengele kwa hivyo tutaanza kwa kuenda kazi kidogo.

Sura ya sita ni juu ya uwakilishi wa watu. Sehemu ya kwanza ni utaratibu na upigaji wa kura, inazungumzia juu ya kanuni za jumla, inazungumzia pia juu ya uchaguzi, inazungumzia haki ya kupiga kura, sifa za mtu kusajiriwa na kutostahili kufanya nini? Kusajiliwa. Zinaeleza juu ya kupiga kura na zinaeleza pia juu ya ugombeaji bila kupingwa.

Ningetaka kuzungumzia maneno mawili tu kwa kirefu kidogo juu ya hiki kipengele na ya kwanza ni juu ya mpango wa kupiga kura. Wakati huu tunapiga kura yenye inadhiwa first through the votes, yule wa kwanza kupitia kwenye voti ndio mwenye anashinda. Yaani kupiga kura mtu mwenye atapata kura nying zaidi ndio mshindi. Tulipoluwa tukienda kupata maoni, watu wengi walitueleza juu ya maeneo ya ubunge na tulikuwa na malalamiko nyingi sana. Watu wenye wanatoka pahali yenye watu wengi, densely populated walituambia kuwa kikao cha kupigia kura ama cha Kibunge kiandaliwe kwa kadili ya nini? Ya wingi wa watu na tusifikirie jambo lingine isipokuwa wingi wa watu. Tulipoenda Uashi Ngishu, tuliambiwa Trans Nzoia, Murang'a na pahali pote penye watu wengu, Vihiga na pahali kama hapo.

Tulipoenda kwenye makao yenye watu wachache kama Marakwet na Turkana, North Eastern, Wajia, Mandera, Kajiado. Walituambia mkienda kutengeneza habari ya vikao vya Bunge mfikirie tu, eneo kwani maeneo yetu ni marefu sana. Unaweza kuenda mile mia tano ukijaribu kuona Mbunge wako kwa hivyo msifikirie wingi wa watu kamwe, mfikirie tu eneo. Waliotuambia tuangalia eneo walikuwa watu wa wapi? Wakenya na waliotuambia tuangalie wingi wa watu walikuwa watu wa wapi? Wa Kenya. Na sisi tulikuwa Tume ya nani, ya watu.

Sasa tumepata hayo mambo mawili tumependekeza hivi, kuwa tuwe na utaratibu tulionayo hapa lakini tuchanganye na utaratibu mwingine. Utaratibu wa kusema kuwa kama hapa Eldoret North ni chama kipi kilichokikubwa kuliko zile zingine?

**Audience:** KANU.

**Com. Salome Muigai:** Ninakiuka haki zenu za maoni. Nataka wananchi wenye kupiga kura hapa kwani nyinyi mmetoka sehemu mbali mbali. Ni chama kipi kilichokikubwa? Ziko sawa, gani na gani basi ni sawa? KANU na...

**Speaker:** KANU na NAK.

**Com. Salome Muigai:** Tuache NAK hatujapigia NAK kura bado. Ni KANU na DP. Haya, sasa tunasema hivi, mpiga kura ukija utapiga kura mara mbili, utapigia Mbunge wako mwenye unataka na utapigia chama. Utapiga kura ngapi? Mbili. Sasa kura ya Bunge yoyote atakayepata kura zile nyingi ataenda Bunge lakini kura ya chama unaweza kumpigia Mbunge wako na chama chake ama unaweza kusema, mimi nampenda fulani tunajua ni mtu mzuri lakini hicho chama chake sikipendi. Kwa hivyo naenda kupiga kura moja kwa Mjumbe na kura ya chama kwa chama tofauti.

Hizi kura zikiwekwa pamoja kile chama chenye kura nyingi zaidi kitapata viti vingine vya ziada. Hii itafanya nini? Itakubalisha wale watu jamii ya wadogo wapate Mjumbe wao lakini vile watu wengi pia watapata Wajumbe zaidi ndio waweze kuwa balanced.

Jambo lingine la hizi kura za ziada ndio inaweza watu wengine wa ziada ambao ni nominated MPs, si nominated, kila chama wakati wa kuleta candidates wao wataleta pia majina ya watu wao kusema kukipata viti vingine ishirini watu wetu ni fulani na fulani na fulani. Na watakuwa wanapigia kura kwenye chama juu ya majina hay, they will be elected and they will come from the party. Jambo la kwanza la hii ni kufanya usawa wa vote.

Ya pili ni kuwa ile jamii kubwa ikishapata Mjumbe wao inaweza pia kwenye hiyo wilaya ama kwenye hiyo eneo kuhusisha vikundi vingine vya watu walivyo wadogo na wangetaka kulete kwenye utawala. Kwa mfano ikiwa ni Eldoret North, Mjumbe wa leo ametoka wapi na anaitwa nani?

**Audience:** Ruto.

**Com. Salome Muigai:** Ni wa jamii gani?

**Audience:** Kalenjin.

**Com. Salome Muigai:** Ya Kalenji na Eldoret North kuna makabila mengine gani? Kuna Kikuyu, Luo, Luhya, Wahindi. Kwa hivyo KANU ikipata viti vingine vitatu kwa ajili wa wingi wa kura zao wana nafasi sasa ya kusema vile tumeshapata Mbunge kutoka jamii ya Kalenjin hiki kiti kimoja tunapatia jamii ya Wahindi kwani ni ndogo kabisa lakini inashirikisha uchumu wa eneo letu. Hiki kiti kingine tunaweza kupatia mtaalam kwani sisi watu wa Eldoret North ni wakulima si hivyo? Na watu wenye tumepata kwenye Bunge ni wanasisia na hakuna mtaalam wa kilimo. Kwa hivyo kura yetu moja ama kiti chetu kimoja tutapatia nani? Mtaalam wa kilimo ndio basi tukianza kuchangia Bunge alete utaalim katika mijadala ya kilimo.

Kwa hivyo hivi viti vitaleta wataalam, vitaleta jamii ndogo, vitaleta akina mama na pia tumaweza kusema tumepata nchi nzima

kama tusema KANU, tumepata watu wote wasio na ulemavu. Kwa hivyo kama tuna kiti cha ziada tunaweza kuleta mlemavu mmoja hapa au wawili.

In other words, mtu akiangalia Bunge letu lenye litakuja kwenye hii Katiba tungetaka aone sura ya Kenya. The people of Kenya. If we have are men and women in Kenya our Parliament will have men and women. If we have small communities like Ogiek in Kenya we should use this strategy to bring them to Parliament. So that is the whole idea for the 90 seats.

The other question is, why are we saying that half of these seats should be given to women. Because we have said in our values that any elective group much have what number of women?

**Audience:** A third.

**Com. Salome Muigai:** A third. If we took all men then the Bunge will not be constitutionally balanced. So we are looking for ways of ensuring that when our Parliament for the first time it is reflecting the face of Kenya and it is meeting the constitutional needs. Hiyo ndio lengo la kwanza lenye ni kipya kwenye hii mapendekezo ya Katiba. Lakini ni kuwa zamani tulisema kuwa mtu akiwa hajapingwa basi eneo lake halikupiga kura, lakini kwa ajili sasa kila chama kitahitaji kuhesabu kura zake za pamoja ni lazima hata pahali yenye hakuna upingamizi kupigwe kura. Ni hayo mawili ndio nilikuwa nataka kueleza.

Tuende kwa sehemu ya pili yenye kuzungumza habari ya Tume ya Uchaguzi, vile itakavyoundwa, majukumu yake, wafanyikazi wake na mipaka ya maeneo ya Bunge. Mambo mawili ningetaka kusema juu ya hili Tume. Kwanza tumepungua Wanatume, tumesema kuwa hili Tume litakuwa na Wanatume wasiopungua wanane na wasiozidi kumi ili iwe Tume ndogo yenye inaweza kufanya kazi zake vilivyo. Ikihitaji watu wengi zaidi iajiri watu wake so that there is ....not a big Commission.

Neno la pili ni kuwa tumeiongeza jukumu nyingine moja. Tumesema kuwa Tume ya uchaguzi ndio yenye inafuata mambo ya kisiasa na vile tunavyofanya kazi zao wakati wa uchaguzi. Kwa hivyo tumeita kazi ya ku-register na de-register vyama vya kisiasa kwani hao ndio kuona vyama vya siasa vyenye nidhamu na vyenye hazina nidhamu. Kwa hivyo badala ya hao kuenda kushtaki hizo vyama kwa mtu mwingine hao wenyewe watakuwa na jukumu ya kusajirisha ama kutosajirisha vyama vya kisiasa.

Sehemu ya tatu inazungumzia habari ya vyama vya kisiasa na inasema haki ya kuunda chama cha kisiasa, wajibu, utajirishi, sifa ya chama kusajiriwa, hali ya shirika, usajirishi, kufungwa na mambo mengi ya vyama vya siasa. Jambo moja tu ningetaka kuzungumzia juu ya jambo la vyama vya viasa zingine mtasoma. Tumesema vyama vya siasa vipatiwe fedha za uma kwani malalamiko mengi imekuwa kuwa vyama vya siasa hazitoshani na uwanja wa kuchezea hiyo kandanda wanaocheza haukosawa kamwe. Watu wengine walituambia kuwa vyama vingine vinakuwa uwanja umeunika sana upande wao wa kupigia mpira wao upande ule umeenda moja kwa moja kwenye goal ya vyama vile vingine kwani uwanja haujasawawishwa hata kidogo.

Kwa hivyo tumesema vyama vipatiwe pesa za uma lakini je, kuna masharti yoyote? Ndio. Sharti ya kwanza, lazima hicho chama kiwe kimepata 3% of the national vote. Kwa hivyo tukisema hivyo wakati huu tuna vyama vingapi? Hamsini na zaidi, sivyo? Lakini tukiweka kwa hii kichungi cha 3% of the vote zote zitabaki? La na tena vyama vyenye vinataka pesa za uma lazima vionekane pia ni vyama vya kitaifa. Hatutaki kupatia vyama vya kikabila mali ya uma kwa hivyo hii pia ndio nafasi yenye itafanya chama chenye kiko na watu pengine kutoka Central Province na kuna viti vingine vya ziada venye tulizungumzia badala ya kuchagua mtu wa Central Province kutoka central Mjumbe ndio ionekane zina sura ya kitaifa. Haya ndio mambo yenye tumejaribu kuweka kujaribu kusawawishana mambo ya vyama vya kisiasa. Haya mambo mawili tu ndio yenye nitazungumzia zingine tafadhali mtasoma kwani hii ni sura yenye mambo mengi.

Sura ya saba, mkikubali nitakunywa maji ingawa zitampa kila mtu. Sura ya saba inazungumzia sheria. Sehemu ya kwanza inazungumzia habari ya Bunge, habari ya kuundwa kwa Bunge, wajibu wa Bunge, kuharishwa na uteuzi wa Bunge, idhini ya matumizi ya fedha ta Bunge yaani Bunge na jukumu zake. Halafu sehemu ya pili inazungumzia muhundo na wanachama wa Bunge. Kwa Bunge ya jumla ningetaka kusema hivi, kuwa Bunge linalopendekezwa kwa hii Katiba ni Bunge lenye litakuwa na vikao viwili. Kutakuwa na kikao kile cha Bunge cha kawaida ya watu wenye wamechaguliwa, lakini pia tutakuwa na kikao kingine tunaita Baraza la Taifa. Hili baraza itakuwa na Mjumbe mmoja kutoka kwa kila Wilaya, hiyo itatupa Wajumbe wangapi? Sabini hivi ama karibu na sabini. Tutakuwa na viti vingine thelathini vyenye tumependekeza zitakuwa za akina mama.

Mwanzo mwanzo kutakuwa shida kubwa kufikiria ukiuliza Uashingishu watupe Mjumbe mmoja kuwa mama. Nafikiri ni Wilaya ngapi zenye zitatupa mama. Ukiuliza tu Mjumbe mmoja kutoka kwa Wilaya nafasi ya kupata mama ni kubwa? Si kubwa sana.

Kwa hivyo tumesema kila Wilaya itatupa Mjumbe mmoja halafu kila mkoa itatupa akina mama wane, halafu Nairobi watakua wawili. Kwa hivyo hiki kikao kitakuwa na Wabunge mia moja sabini waliotoka kila Wilaya na akina mama wanne kutoka kwa kila Mkoa. Hii kazi ile kubwa yenye hiki kikao ni kuwa check and balance ya Bunge kwani tumeipa Bunge madaraka mengi, tumesema Bunge itawasiliana na vyama na Rais wakati wa kuchagua watu yake kama kuchagua Mahakimu atawasiliana na Bunge akichagua watu wengi na mambo mengi atawasiliana na Bunge. Lakini pia Bunge inaweza kuwa na uhuru iliona kikomo, kwa hivyo naye Baraza la Kitaifa itakuwapo kupunguza kazi ya Bunge, checks and balances within the division of power.

Sehemu ya tatu inazungumzia maofisa na wasimamizi na watenda wengine kwenye kikao hivi viwili vya Bunge, na sehemu ya nne inazungumzia sheria na utaratibu wa Bunge.

Sehemu ya tano ya sura hiyo ni kikao na ratiba ya Bunge na tuliambiwa kika pahali kuwa ratiba ya Bunge itengenezewe wapi, na Bunge lenyewe. Parliamentary callender should be the responsibility of Parliament itself. So this tries to put in strategy on how this can be fabricated.

Sehemu ya nne tumeelezwa uhuru wa kuzungumza wa Wabunge, uwezo wa fadhila na kinga. Protection of the immunity of the parliamentarians na ways of involving the public in the parliamentary debate. Vile tutashirikisha uma na kushirikishwa kwenye kazi za Bunge. Pia tumeweka Tume ya uduma za Bunge kwenye katiba. The Parliamentary Service Commission has been entrenched in the new Constitution.

Sura ya nane inazungumzia mamlaka ya nchi, the Executive, inazungumzia sehemu ya kwanza kanuni na mifumo ya mamlaka ya taifa. Sehemu ya pili inazungumzia habari ya Rais na makamu wake.

Ningetaka tuzungumzie kidogo habari sana sana ya kifungo cha kazi za Rais kwani kuna tunasipoweleka na watu wengi wanasema Raisi hana mamlaka tena na hii ndio ukweli kabisa. Lakini kabla ya hayo ningetaka kuzungumzia kwamba Rais ama mtu yoyote atakayesimama kuwa Rais atasimama na mwenzake na huyo mwenzake atakuwa running mate. Wote watachaguliwa moja kwa moja na wananchi na akishachaguliwa huyo mwenzake atakuwa makamu wa Rais na huyo makamu Rais atashikilia Urais wakari Rais hayuko.

Majukumu ya Rais wa taifa ni kipengele cha 111, Rais atazungumzia uvumbizi wa kila bunge na ilivyochaguliwa kulingana na ibada ya 141. Rais pia atakuwa na kikao maalum cha Bunge mara moja kwa mwaka kulingana na ibada ya 14. Ibadia 14 inasema Rais kila mwaka ataeleza taifa tuko mahali gani kwenye kipengele ya sura ya tano, haki za uhuru kwa wananchi. Nafasi hiyo ya pili inasema anaweza kurudia Bunge wakati mwingine wowote na anaweza kulivunja Bunge tu katika hali iliyotajwa kwenye ukurasa ya arubaine na mbili. Kwa hivyo haya mambo mengine mtayasoma baadaye.

Rais atateuwa na pengine kwa mjibu wa Katiba (b), anaweza kuteuwa na kutimua lakini kwa utaratibu wa Katiba. Anaweza akawaajiri, Waziri Mkuu ambaye atakuwa ndiye kiongozi wa chama cha siasa. Inazungumza pia kuungwa mkoni na watu wengi bungeni na manaibu wawili wa Waziri Mkuu ndio itakuwa kazi ya Rais kuwateuwa zaidi ya Mawaziri wangapi? Kumi na tano na wasaidizi wao kumi na tano pia. Pia Rais atateuwa maafisa wa mahakama, afisi yoyote ya uma ambayo katibu inataka Raisi amteuwe. Majukumi zingine nyingi mpaka mwisho wa hiyo ukurasa. Ningetaka tafadhali kila mtu awe na nafasi ya kusoma.

### **(Interjection)**

Can we have Emmy? Could you please pick up the paper of their lists so that everybody don't just come and go.

Hiyo ya ziada ni kuwa, there will be dialogue, there will be consultation, with certain groups of people or certain institutions. We had created avenues of more consultation so that more people are involved in whatever it is that we are doing in this country.

Ya tatu ni juu ya waziri mkuu na baraza la mawaziri nimeeleza kuwa tayari tutakuwa na Waziri Mkuu atakuwa na Manaibu



wawili. Watachaguliwa kutoka Bunge, kutoka kwa chama chenye Wabunge wengi zaidi. Baraza la Mawaziri itatolewa nje ya Bunge kwa sababu hizi. Tumesema na wananchi kuwa Mbunge wao akichaguliwa kuwa Waziri hamwoni tena mpaka siku ile yeye na Rais wataenda kutembelea constituency hiyo. Pia wananchi walisema kuwa wakati mwingi Wabunge wengi wanaogopa kuwatetea kwani bado wanangoja kuteuliwa Mawaziri, kwa hivyo wanakosa kufanya jukumu yao hasa wakiwa wametoka kwenye chama tawala kwani wanangoja kuteuliwa, kwa sababu kila siku unasema hiyo babarabara wakati mwingine hautapata kuteuliwa. Kwa hivyo Mbunge anakosa kuwakilisha watu wake vilivyo.

Jambo lingine lenye watu walitumbia ni kuwa kuna watu wengi Kenya pia wenye kutaka kazi, kwa hivyo kila mtu mmoja apate kazi moja. Lingine, watu walikuwa na mambo mengi ya kusema juu ya hili jambo. Wakisema kuwa Wabunge ... (nimesahau neno lingine lakini nikikumbuka nitawaeleza, wacha niendeleo na habari ya Baraza la Mawaziri. Wengine walisema kuwa wanataka Waziri wenye ni wataalam, professionals. Mtu akiwa Waziri wa Elimu lazima awe Mwalimu, akiwa Waziri wa Afya lazima awe Daktari, akiwa Waziri wa Kilimo lazima awe Mkulima ama Agricultural Profession, awe yeye ni Veterinary ama nini. Waziri wa Defence awe ni Askari ama anapata ofisi hiyo. Kwa hivyo watu wengi walisema wangetaka utalam uletwe katika kutimiza ama kuendeleza Wizara hizo. Nafikiri nitamalizia hapo juu ya Waziri Mkuu na Baraza lake la Mawaziri.

Sura ya tisa ni mfumo wa Mahakama na sheria. Sehemu ya kwanza inazungumzia juu mfumo wa Mahakama. Kile chenye ningetaka kueleza hapa tumeyajua habari ya wenzetu wa Mahakama, uhuru wa Mahakama, Mahakama ya Juu. Ni kuwa mependekeza tuwe na Mahakama ya juu yaani Supreme Court na hii itakuwa na kazi mbili. Ya kwanza ndio itakuwa koti ya Kikatiba, mtu yoyote akiwa na shida na Katiba ataenda kwenye Supreme Court kuuliza habari ya Katiba.

Pia Rais anaweza kuomba Supreme Court kuangalia habari ya Katiba. Halafu tutakuwa na Mahakama hizi zingine kama Mahakama ya Juu, Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu yaani High Court na itakuwa tumeeleza juu ya utaratibu wa kuteuwa Mahakimu, sifa anayestahili kuteuliwa, awamu ya Ma-Judge ofisini, kuondolewa ofisini, Mahakama ndogo na pia tumezungumzia Mahakama ya Kadhi. Mbeleni tulikuwa na Mahakama ya Kadhi kwenye kiwango kimoja sasa tumeifanya Mahakama ya Kadhi kuwa viwango tofauti.

Sehemu ya pili inazungumzia juu ya mfumo wa sheria. Tumeambiwa na wananchi wengi kuwa Attorney General anakazi isiyofahamika, mara moja yeye ni Mbunge, mara ya pili yeye ni Mawaziri kwani anakaa kwenye Cabinet, mara ya tatu yeye ni Mshauri Mkuu wa serikali kisheria, mara nyingine yeye ni Mshataki Mkuu na hii mambo yamekuwa mengi sana machanganyiko kwenye ofisi moja na ofisi moja. Kwa hivyo hii ofisi tumeigawanya mara mbili, kutakuwa na ofisi, hata akiambiwa kuwa yeye ndio Mkuu wa Sheria, yeye ni Mwanasheria Mkuu kwani hakuna mtu mkuu kuliko sheria. Kwa hivyo tumeigawanya ofisi ya Mwanasheria Mkuu na ile ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Uma ili tuwe na ofisi mbili.

Tumependekeza pia ili wa Uma, the Public Defender. Hii naye kazi yake ni kuangalia pahali gani haki zako zimekeukwa. Na tumezungumzia pia habari ya uwezo wa kuhurumia na nani atayehusishwa.

Sehemu ya tatu ni taaluma ya sheria na hiyo itakuwa ndio mwisho wa hiyo sura ya tisa.

Sura ya kumi inazungumzia juu ya uvungazaji na usambazaji wa madaraka yaani devolution. Hii ni nafasi ndefu kabisa ina ukurasa tofauti. Ningetaka tujue maneno mawili ama matatu juu ya vile tuliambiwa na watu. Wananchi walituambia kuwa serikali ya Nairobi iko mbali sana nao wangependa serikali ya karibu na sasa tumependekeza kuwa kutakuwa na serikali la kila kijiji, kutakuwa na serikali katika kata lakini ile serikali kubwa ya watu yenye iko karibu nao itakuwa Serikali ya Wilaya. Hii Serikali ya Wilaya itakuwa na Bunge lake na itakuwa na sheria zake zenye kuhusu hiyo wilaya. Kwa mfano, ikiwa serikali ni ya Uashi Ngishu mambo ya muhimu ya Uashi Ngishu itakuwa nini? Kilimo, lakini serikali ya Wilaya ya Kajiado mambo ya kwanza yake itakuwa ufugaji. Kwa hivyo kila serikali itakuwa na nafasi yake ya kuweka maanani ama kiwe kibao mbele mambo yake ya muhimu yenye itakuwa na tafauti.

Pia kutakuwa na Serikali ya Mkoa lakini Serikali ya Mkoa kazi yake itakuwa ya coordination na coordination ni kufanya nini? Kusimamia ndio ku-coordinate.

**Speaker:** Kuunganisha.

**Com. Salome Muigai:** Kuunganisha, itakuwa kuunganisha Wilaya moja na nyingine. Kwa mfano ikiwa watu wa Wilaya ya Uashi Ngishu wana mahindi wasijua la kufanya nayo vile ilivyonyingi. Watu wa Kajiado wamekuwa na ukame hawana chakula, basi itakuwa kazi ya Serikali ya Mkoa kutafuta soko Kajiado ndio wanunue mahindi ya Uashi Ngishu. Nao pia watu wa Uashi Ngishu mara nying ufugaji wao ni wa ngombe wa maziwa kwa hivyo hawana ngombe nyingi za nyama hata akizaliwa wanauza ama wanachinja. Kwa hivyo wakati mengine hiyo Serikali ya Mkoa itaweza kuwafatutia wafugaji wa Kajiado soko la nyama katika Uashi Ngishu na mambo kama hayo.

Bunge la Wilaya litachaguliwa kwenye Wilaya lakini itafuatilia Katiba yaani kila mara mmekubaliana Katiba lazima zije mpaka wilayani.

Sura ya kumi na tatu inazungumzia juu ya fedha za uma, ile kodi zinatoshwa na vile mambo yote serikali inaipotumia, nani mwenye kuidhinisha pesa zipi, wakati gani. Mambo mawili ningetaka kusema juu ya matumizi ya fedha.

Ya kwanza, hakuna mtu atakayekubaliwa kukosa kulipa kodi, no exception. Lakini kukiwa ni lazima mtu asilipe kodi lazima baada ya muda fulani mtoza kodi aeleze Bunge ni watu wangapi na akina nani wenye waliokolewa wasilipe kodi, kwa sababu gani na ilikuwa ni kodi ya pesa ngapi. Ndio akisema tulimpatia Salome alete gari bila kulipa kodi kwani alikuwa na ulemavu, watu wa Uashi Ngishu watasema sisi tumemjua Salome tangu alipozaliwa, tangu huko Township, hiyo ni kweli ama hiyo ni uongo kwani habari itakuwa wazi kwa kila mtu kuyaona. Hiyo ni jambo la kwanza.

Jambo la pili ni kuwa, tumeliunganisha na kuunganisha malipo ya kodi na hudumu zenye watu wanapata. There is a linkage between the taxation and the services that are supplied. Hayo tu ndio mambo mawili yenye nilikuwa nataka kueleza kwenye hiyo sura ya kumi na tatu.

Sura ya kumi na mne ni juu ya Huduma za Uma yaani public service. Tumeangalia tena Public Service Commission ama Tume ya Huduma ya Uma, tumeyapa mamlaka na wajibu wao, tumeleta uteuzi wa maafisa nani atakayechaguliwa na atakuwa amehitimu aje.

Sehemu ya pili yenye ni pia huduma ya Polisi ya Kenya, hii yenye tutachagua mkiuliza maswali yote tuliyoko nayo kuhusu polising, habari ya kuajiri, ni nani mwenye anaajiriwa. Na hivi Tume zote kila mmoja itakuwa nafasi ya kutoa repoti yake kwa Bunge zingine mara moja kwa mwaka, zingine mara mbili ama mara tatu kwa mwaka kulingana na kazi zao.

Sehemu ya tatu ni juu ya huduma ya Kenya ya Kurekebisha Tabia. Kwa hivyo kuna Tume ya Huduma ya uma, kuna Huduma ya Polisi wa Kenya na pia kuna Huduma ya Kenya ya kurekebisha tabia yaani prison.

Sura ya kumi na tano ni juu ya Kikosi Cha Ulinzi wa Usalama wa Taifa. Hiki kikosi Mwanakiti wake atakuwa Rais wa taifa. Kwa hivyo hii pia ni mamlaka mapya kwa Rais na pia tukisoma hayo tutasikia ni nani mwenye atakuwa kwenye hizi baraza, atachaguliwaje ama ataapishwa vipi ofisi yake. Kila pahali yenye tumeweka utaratibu wa kuajiri pia tumeweka utaratibu wa kufuta.

Sura ya kumi ni sita ni Uongozi na uaminifu. Wanakenya wengi walituambiwa kuwa haitoshi kuwa mtu amehitimu masomo ingawa tungetaka wenye kutuongoza wawe na masomo kiasi fulani pia ni lazima wawe watu waminifu, tabia zao pia zichunguzwe. Kwa hivyo tumeweka Tume yenye itachunguza tabia na maadili ya mtu yoyote atakayetaka kusimama kuwa kiongozi wa nchi hii ama wa Jamhuri.

Sura ya kumi na saba ni Tume zenye tumeanzisha Kikatabi, sijui kama tulizungumzia kwenye utangulizi ama pahali fulani yaani itakuwa taifa lenye kufuata sheria. (Na mnasikia vile itakuwa na shida? Sheria moja tu tuliofikiria kwenye hii jamhuri ndogo yenye iko kwenye hiki chumba ndio mnaona pia tunashida ya kuifuata hiyo sheria yetu).

Sura ya kumi na saba inaeleza juu ya Tume zenye tumeanzishwa Kikatiba kwanza tumeeleza kwa jumla, tume Zitaanzishwa vipi, watu gani wataweza kuketi kwenye Tume, Tume zinamajukumu gani, Tume zinawajibu gani, Tume zitapatiwa fedha kutoka wapi? Kila tume yenye imeanzishwa ya Kikatiba. Halafu tumezungumzia Tume zingine lakini Tume zenye hatujawaeleza habari yake ni kama Tume rasmi ya Katiba. Kuna tume yenye tutaipatia kazi kwa miaka mitano tu, baada ya miaka mitano lazima iwe imetuwezesha sheria zote kubadilishwa kuandamana na Katiba mpya, baada ya miaka tano haipati nafasi nyingine ya kuendelea.

Tume ya Kuajiri Walimu pia tumeweka kwenye Constitution. Na tumeanzisha Tume ya Mishahara na malipo yenye itaangalia mishahara ya wafanyikazi wote wa uma kuanzia kwa Rais mpaka kwa yule mwingine aliwe kiwango kingine chochote ili kuhakikisha kuwa mtu mmoja...(tuliomba tafadhali funga mobile kwa wenye wamekuja wamechelewa). Hii Tume ya mishahara na malipo litahakikisha mtu moja hapati shilingi milioni tano na mwingine kupata shilingi mia tano na wakienda kununua mali ya uchumi wanauziwa bei moja. Watu wengi walilalamika habari ya mishahara na tukaomba hiyo si kazi yenye inaweza kufanywa kwa muda mfupi kwa hivyo badala ya sisi kuanzisha...

**(Interjection)...**

**Mzee:** Watoke nje.

**Com. Salome Muigai:** Mzee amazungumza tafadhali funga hiyo mobile ama usikiliza ukiwa nje ukimaliza tafadhali uje tena.

Hiyo Tume ya Mishahara basi nimezungumzia. Kutakuwa na Tume ya Uadilifu na Uamini hii ndio tume itakayochunguza kila mtu mwenye kutaka kusimamia cheo chochote cha uongozi. Tume ya haki za binadamu na haki za kiutawala ndio nilisema mbeleni kuwa itakuwa Tume ya kuangalia matakwa yasio ya kamwe, ya haki na huru. Itakuwa na nafasi moja ya kuangalia haki za kijinsia yaani gender issues, itakuwa na Mwanatume mwenye atakuwa anaangalia mambo ya watoto, itakuwa na Mwanatume mwenye kuangalia haki za watu wenye ulemavu.

Niliulizwa jana kwa sababu gani hakuna haki za wanatume. Haki zote zilizobaki baada ya za walemavu, wanawake na watoto, hizo zingine zote zenye ziko kwa Katiba yetu ni za akina nani?

**Audience:** Wanaume.

**Com. Salome Muigai:** Sura ya kumi na nane inaeleza juu ya badilisho la Katiba na badilisho la Bunge na haki ya utivu. Hiyo ni sura yenye kila mtu inambidi kusoma kuangalia matakwa yake.

Sura ya kumi na tisa ni ufafanuzi ya mambo yenye tumezungumzia yaani transition. When we say this what do we mean? Kitu chenye nimejifunza kwenye utaratibu huu ni kuwa sheria inakikomo chake, kuna mambo mengine yenye unatakiwa ufanye ile sheria inakurusu.

Kwanza watu wengi walituambia hii uhuru wa kuamini na kuabudu ni lazima tuseme ni lazima tuseme ni kuabudu ama kuamini Mungu wala sio shetani. Lakini kisheria ukisema kuabudu Mungu lazima ufafanue Mungu ni nani. Ukisema mtu asiabudu shetani, lazima ufafanue shetani ni nani. Na tulikuwa na shida kubwa sana kufafanua kuwa Mungu ni nani na shetani ni nani. Kwa hivyo vile tulifanya ni kuacha uhuru wa kuabudu lakini tukasema sheria za Bunge zenye ndio sheria tekelezi na pia sera,

policies zitaweza kueleza vitu gani zenye hatuwezi kufanya kwenye huo uhuru wa kuabudu. Basi ndizo pengine zitatolea mazoezi yenye watu wengi walitupa ya kuonyeshana kuwa pengine mtu anaabudu Mungu.

Sura ya ishirini, kanuni za mpito na matokeo ni kuonyeshana ile utaratibu wa kugeuza kutoka kwa hii Katiba tulio nayo kuenda kwa Katiba mpya ili pasiwe pengo na pasiwe mtu kudhulumiwa ama kusia kuwa masilahi yake hayakuwekwa mahanani. Kwa hivyo hiyo sura inaongezea mambo yenye tunataka kuangalia wakati huu wa kipindi kifupi. Kuna mambo yenye iko kwa hii Katiba yenye haitafanyika kwa mwaka moja ama miwili ama mitatu ama mnne, lenye itachukua pengine miaka tano. Kwa hivyo hiyo sura inaonyeshana vitu gani viko katika transition time na mwishowe pale nitaongezea mambo mengine kama kiapo yenye tulizungumzia, kama map ya Kenya na mambo mengi kama hayo.

Kwa hayo mengi kwani haikuwa machache nataka kuwashukuru kwa kusikiliza habari ya safari hii ndefu ya Katiba ya Kenya. Asanteni sana. (*Applause*)

Sasa kuna watu wenye walikuwa na maswali na nitasema kuwa nitachukua maswali wakati wa mwanzo ama katikati. Vile nitafanya nitampa hiki kipasa sauti, nitampa mwenzangu Juma ili nipate nafasi ya kupunzisha sauti yangu halafu nitachukua maswali kutoka kwa watu kumi hivi. Utauliza swali lako nami nitaliandika chini halafu badala ya watu kumi kuuliza ama watu saba ama watu fulani nitayajibu hayo maswali kwa pamoja.

Ningetaka tafadhali mniulize maswali ya ufafanuzi peke yake yaani clarification points, msiniulize Bunge likivunjwa kesho tutafanya nini? Your guess is as good as mine. Kwa hivyo mniulize mambo yenye ninaweza kujibu ama uweze wa kujibu.

**(Interjection)**

**Moses Keter:** Excuse me please. You know we have our land problems in this area and ...

**Com. Salome Muigai:** Nilisema nitampa Juma, just one moment. Let me explain how we are going to do it. I am going to give the mic to Juma to be the Chair and people are going to raise up their hands and I would want you to come in front here because we don't have a mic that can move. Utakuja hapa, utazungumzia kwenye mic na pia tutaandika majina yako ili wakati tutakapoleta maswala haya kwa Tume ikuwa na watu wenye waliuliza pia. Mr. Juma please take up this chairmanship.

**(Interjection)**

**Moses Keter:** You skipped chapter 11.

**Com. Salome Muigai:** Oh, I did, I don't talk about it, sorry thanks. I am sorry how could I not. Chapter 11.

Sura ya kumi na moja inazungumzia habari ya ardhi na mali. Kila pahali yenye tulienda kulikuwa na shida za ardhi na mashamba

lakini kuna mambo matatu yeye hii Katiba mpya imependekeza.

La kwanza ni kuwa ardhi yote ya Kenya ni ya watu wa Kenya, tumeiondoa kuwa ardhi ya jamhuri, ardhi ya serikali na tukasema ardhi ni ya watu wa Kenya. Tukasema ardhi itamilikiwa kwa njia tatu, kutakuwa na ardhi ya kibinafsi na tutakuwa na ardhi ya jamii (community) na tutakuwa na ardhi ya uma, kwa hivyo ardhi itamilikiwa kwa njia tatu.

Jambo la tatu lenye ningetaka kueleza juu ya ardhi ni kuwa shida zenye tulikuwa zilikuwa nyingi na hatungeweza kutatua kwa miezi mitatu au mnne yenye tulikuwa nao ya kutengeneza huu mswada. Kwa hivyo pia tumeweka Tume ya ulinzi wa mali katika haki. Hiyo Tume ndio yenye itachunguza, tumeiweka kwa Katiba so that it is entrenched in the Constitution na kazi yeke itakuwa kuchunguza shida zilizoko za ardhi na makao. Na itakuwa ikiendelea lakini hii, tofauti yake pengine ile iliyoko ni kuwa itahitajika kutoa repoti yake kwa Bunge and by extension kwa kila moja wetu mara tatu kwa mwaka.

Halafu la ziada ni kuwa tumesema mambo mengi yatakuwa yakitolewa kwa Bunge, kwa hivyo nayo Bunge tumesema kuwa miswada na majadiliano yao itachukuliwa na vyombo vya habari moja kwa moja ili wakati wanaposikia hizo repoti sisi kama wananchi tusipate moja kwa moja.

Asante.

**Dan Juma:** Asante sana Commission for that very good presentation. We will have 10 questions from those who want to ask questions. I will give this opportunity to the Coordinator to take the first 10 questions.

**Gilbert Bor:** Basi watu ambao wanataka kuuliza maswali hii ni nafasi yenu na mmesikia vile tumeelezwa na Commissioner kwa ile draft ni hali ya kujaribu kuelewa kila sehemu ya hiyo draft na mambo mengi mtasoma kwa hiyo draft. Kwa hivyo maswali tunatarajia iwe ni maswali ya mambo ambayo hauelewi katika hiyo draft na kama ni recommendation ingefaa iwe in summary na baadaye uandike iende Nairobi ili iweze kujadiliwa katika National Conference.

**Com. Salome Muigai:** Let me explain what happens from here. Nilisema kuwa kazi yetu ya kwanza ilikuwa kuchukua maoni kutoka kwenu halafu tuifanye kuwa report na reporti hizo ziko hapa halafu jambo moja yenye nilisema ni kuwa, tumetengeneza hata reporti ya kila kikao cha Bunge. Kwa hivyo kama unataka kujua watu wa Eldoret ya Kaskasini walituambia nini, ukienda kwa ofisi ya Coordinator utapata hiyo reporti ya kutoka hapa kikao hiki.

Mkondo wa pili tukitoka hapa baada ya kutengeneza huu mswada na ripoti hizi ni kuja kuwarudishia hii mswada, what I have just done ili msikie kama vile the delagete from the back amesema kuwa sisi tulieleza sana shida za ardhi na haujazungumzia. Yaani uangalie kama mambo yenye mlituambia yameingizwa kwenye mswada. Hii mswada inatakiwa kufanyiwa debate na nyinyi, mnaweza kuzungumza na mtu mmoja, unaweza kuzungumza na watu kumi, ukiwa una kikundi chako, tafadhali

wapelekee hii habari uliojua leo ndio mzungumzie. Mkiona kuna mambo yenye ungetaka kubadilisha ama ungetaka kuongeza mtaandika halafu mtawapa watu wenye watawakilisha kwenye kikao cha taifa. Kikao cha Taifa cha kuzungumzia hii Katiba itafanyika tarehe ishirini na nani na kutakuwa na wakilishi watatu kutoka kwa kila Wilaya na tungetaka wakilishi wenu wasimame ili mwaone tena kuna wengine wamekuja hapa wamechelewa. Tafadhali mnetaja majina?

**Moses Keter:** Moses Keter.

**Emmy Kiprop:** Emmy Kipsoi Kiprop.

**Com. Salome Muigai:** Moses Keter na Emmy Kiprop. Kuna mwingine mwenye hayuko leo ni nani?

**Gilber Bor:** Julius Sietenei.

**Com. Salome Muigai:** Julius Sietenei. Hawa ndio wa kutoka Wilaya hii lakini Wilaya ya Uashi Ngishu ina wakilishi wengine wawili wa ziada waliochaguliwa na NGO Council kuna Samuel Tororei kutoka Moi University Medical School na kuna mama mmoja mwenye sijafahamu jina lake.

**Gilbert Bor:** Mrs Hellen Yego.

**Com. Salome Muigai:** Mrs Yego has withdrawn basi akina mama kuna nafasi nyingine side ya NGO Council, kwa hivyo mnawakilishi tano badala ya watatu. Kwa hivyo ukiwa una jambo lenye ungetaka igeuzwe kwa Katiba ama liongezwe, watu wa kueleza ni hao. Mtaandika, mnaweza kuwazungumzia moja kwa moja kama mnawajua ama hamwajuhi, mtaandika mlete kwenye ofisi ya Coordinator yenye iko kwa Kenya National Library hapa Eldoret. Mmepolekee naya atakusanya pamoja na atawapa file wakija ile waje na maoni yenu sio maoni yao wenyewe pekee, pia hao wana maoni yao kwa ajili hao ni Wakenya na ni wananchi kwenye hii Wilaya. Lakini kazi yao kubwa ni kuleta maoni yenu. Kwa hivyo tafadhali mkitoka kama nyinyi mko at the University make your meeting again discuss the issues and bring them to the Coordinators office so that your concerns are brought to the National Constitutional Conference that starts on the 28<sup>th</sup> of this month. Is that understood? Mmeelewa jambo hilo.

Haya je, what happens after that? Kama watu wakikubaliana hiyo Katiba kwenye hicho kikao itapelekwa Bunge na Bunge kazi yake ni kuidhinisha tu iwe Katiba, wanaweza kuikubali yote ama waikatae yote lakini Bunge halijakubaliwa kuenda kufanya marekebisho, hawakubaliwa kuongeza ama kutoa wanaweza kukubali yote ama waikatae yote. Lakini pia Wabunge wote watakuwa kwenye hiki kikao cha taifa. Kwa hivyo pia hao hawa wakiwa na mambo yenye wanataka kuongeza, wataongezea kule.

Watu wakiwa wamekubaliana mambo mengine na hawajakubaliana mambo yale mengine kutafanyika nini? Kukiwa kuna mambo moja ama mawili yenye haijakubalika, itaenda kwa kura ya maoni, itaenda kwa referendum. Hiyo referendum matokeo yake na ile mambo yenye ilikubalika hiyo itapelekwa Bunge pamoja ndio iwe ndio Katiba ile mpya ya Kenya. Sasa tuko tayari kwa maswali ya ufafanuzi.

**Gilbert Bor:** Utaratibu ni kwamba tutachukua watu kumi halafu watakuja hapa mbele, mmoja atauliza swali halafu pia ujiandikishe hapa, mama anaweka recordi ya wale watu ambao wanauliza maswali. Kwa hivyo 1,2,3,4,5,6,7,8,9,10, face the Commissioner and the audience, utauliza swali halafu unapeana microphone kwa the next person na unajiandikisha.

## QUESTIONS

**David Omolo:** Asante sana Commissioner.

**Com. Salome Muigai:** Jina kwanza?

**David Omolo:** Jina ni David Omolo. Swali langu la kwangu ni juu ya serikali ya location, village and provincial government. Jambo lile mimi naona ya kuamba itakuwa mpya kwa generational .....iko yake, kwa hivyo ningependa maelezo zaidi juu ya vile itaundwa. Halafu swali la pili ni kwamba, vile umesoma ya kwamba President hatakuwa mwanachama wa Parliament wala mwanachama wa cabinet je baada yake kuchaguliwa kutatokea Mbunge mwingine au yeye ndiye atakuwa Mbunge wa sehemu yake?

**Wilson Kimaina:** Asante sana Madam Commissioners ambao wamefanya kazi kwa njia nzuri nawapongeza kwa kazi hii nzuri. Kwa hivyo swali langu.

**Com. Salome Muigai:** Jinal lako.

**Wilson Kimaina:** Jina langu ni Wilson Kimani. Ningeliza juu ya hali ya kubadilishwa, lakini nimeelewa hapo. Swali lingine ambalo ningetaka kuuliza, je wageni wale wageni ambao wanarithi arthi katika Kenya, kwa mfano kulikuwa na shamba lingine upande wa East Africa Turning. Niliona watu walijua na haikutaka watu wanunue kwa sababu ardhi hiyo ilionekana ilikuwa ya watu wa Kenya. Walikuwa watu wa jamii ya Kerio ambao ni wakila ya Nandi, hiyo ingekuwa ardhi yao haingewapasa kununua, kwa sababu ilikuwa imemilikiwa hapo mbeleni na wageni.

Swali lingine la pili mimi nauliza juu ya uraia. Mmesema kwamba uraia kama sasa Wamaasai, Turkana au Waborana ambao wanakaa mpakani wanajamii ya nchi ingine na nchi yetu hapa kama Wasomali. Je, uraia huu itakuwaje sasa watu kama wa Asia ambao ni wafanyi biashara wakati tulipata uhuru walikuwa wana uraia wa Uingereza na wengine wakawa raia katika



Kenya. Basi hata hao wanaweza kuwa na uraia wa Uingereza na waendeleo kuwa raia wa Kenya.

Swali lingine nilikuwa nauliza, nilikuwa nauliza Ma-Judge au Mahakama mmesema Judge astaafu akiwa na miaka 65, hapa ningependelea iongezwe kuwa sabini.

Kubadilisha Katiba isiwachiwe Bunge peke yake, lazima maoni ya wananchi itafutwe, waulizwe wananchi kama Katiba tunao ibadilishwe ama hapana. Nafikiri swali langu lingine lipo lakini singeendelea kwa sababu ya nafasi. Asante.

**Com. Salome Muigai:** Sasa ningetaka kuona tafadhali maoni yenye ungetaka ya mabadiliko umpatie coordinator. Yale maswali yenye tutauliza iwe ni maswali ya kufanya tuelewe zaidi vile hii mswada inavyosema. It will take time kwani tukianza kutoa maoni pia, tena na itabidi kukaa hapa mpaka saa kumi na mbili kama vile tulivyofanya wakati wa maoni.

**Juliana Nahumicha:** Naitwa Juliana Nahumicha kupitia C.J.P.C. Eldoret Diocese. Asante Commissioner wetu kwa kazi nzuri Kenya imefanya kuhusu wananchi. Swali langu ni kwamba, tumeambiwa kwamba kulingana na hiyo draft President na vice wake watachaguliwa lakini atafanya namna gani ndio achaguliwe kwa mfano ninaona kwamba nchi hii itaendelea au itatuwekwa katika Katiba kwamba party to propose na pengine wananchi wa-nominate because wakati tunachagua huyu mtu na tunasema yeye ndiye amechaguliwa na kuwa President and if you don't have any alternative it looks like may be that Presidency is only for the few individuals but not for the whole country people will be trying to nominate one.

Swali la pili ni kwamba, wakati tumeona kwamba hii Katiba ikiisha kutakuwa na matarajio au itaendelea kuwa katika mashule. Will it be part of the school curriculum so that we may not go back and become the Wanjiru's of the last milenium or will it be in schools from Primary education upto University so that when one comes forward you know exactly what you need to do at what time and the right time.

Kuhusu kwa mfano, vile tuliambiwa kwamba kulingana na 15, wanatakiwa Mbunge moja wa ziada achaguliwa kuwa mama, are we saying that women are not going to be MPs or what is happening?

Last, this is a challenge to Kenyans today we are making a Constitution and there is a big strike going on. So that, anyone who comes in the next Constitution review, the government should look into it within 3 days if not 7 days so that we don't have a strike taking almost the whole month children are suffering when only 2 or 3 people are enjoying the country's wealth. Thank you.

**Anthony Simiyu:** My names are Anthony Simiyu. I am not understanding how the draft has privilege to higher education in terms of finance and appointment of university officials. I am referring to University that includes high education, you will find that the Vice Chancellors, Lecturers, these people cannot perform their duties independently because there is somebody

somewhere who appointed them. So they are turned into sycophants, how has this draft addressed that issue?

**Victoria Mambo:** Asante sana Bi. Commissioner na watu wote ambao wamefika hapa. Ninamaswali mengi lakini nafikiria nitauliza tu swali moja.

**Com. Salome Muigai:** Utuambie jina lako?

**Victoria Mambo:** Kwa jina naitwa Victoria Mambo.

Swali langu la kwanza ni kuhusu hii maneno ya wanawake ambao umesema one third of the parliamentarians should be women. Ningetaka kujua kama hii Katiba itakuwa implemented soon ama hii maneno ya one third ya wanawake kuenda Bunge watafanyiwa appointment. Hiyo ndio swali langu la kwanza lakini nina maswali mengi sitauliza saa hii vile wakati ni mfupi. Asante.

**Philip Nzei:** Mimi naitwa Philip Nzei. Shukrani kwa makaratasi hii ya Commission ya Kurekebisha Katiba for giving Kenyans a chance to conglomerate in making the Constitution. The first question is on citizenship where we talk about dual citizenship, to be a citizen of Kenya and a citizen and of any other country that is a friend, we know that in the international system, countries can never remain friends, so what will happen to someone who is a citizen of another country then diplomatic relations are cut, how will that happen?

The second question is on the issue of discrimination, this is talking about people should not be discriminated especially on that aspect of age, sex and all that. We know when it comes to even in areas of jobs and all that, a person is told, we don't want a person who is not 35 years of age, that is discrimination, it means that this person is discriminated. I want to know how that has been taken care of because that is part of discrimination in terms of age. The draft says, the President should not be less than 35 years, that is discrimination in itself.

Then the other one on the issue of the death penalty, I will draw some reference to the Bible because I am a Christian. Even the Bible itself gives some threat that if you fail to abide with this law and this law there is some very serious penalty of burning eternally. So I think if we abolish the death penalty here. There are some people to them life on earth is not that much important, they will be committing crimes because they know they will wouldn't be committed to death at all. The death penalty actually affects people's attitude from committing a lot of crime because when you abolish death penalty, you have heard people saying ....(Inaudible) and then also when the Constitution of Kenya says this, they are ready to reduce the morals of people. People will be staying in jail forever.

The most important aspect, another part of my question. We are having the abolision of the Provincial Administration, or rather

we are having the restructuring. What I thought is that, the Provincial Administration is okay, the current structure does not need a lot of structuring. I have written a memorandum and I hope these issues will come up.

The whole issue is, we know the caliber of the people who have been elected to such positions, the crop of Councillors we have in the local areas and we have the same people holding the District Councils and all that and how will that address that, actually in going to achieve these policies with all these elections we have in the location, district and all that. If we allow it from January to January we will be doing the elections. So we realize that on that issue of making the ...when someone is withdrawn or dead from the Councils, we will have re-election again. Tutakuwa na re-election nearly every month and so everybody who is being elected or all these Councils that need elected members, then we might have a lot of incompetence because if somebody is to be elected or when Kenyans election system is that we elect those with materials then we will not elect the marginalized groups. So those people who have property they are going to be elected in those Councils and most of them they don't know anything about administration and most of those things.

Thank you.

**John Ombaka:** Thank you so much, my name is Ombaka Otieno John. I have a few questions to raise first of all I want to talk about the issue of women rights. Now in the Constitution there is the plight of women 'third of we have heard of appointments or elected as members are women. If we have government protecting women rights, in my understanding, a provision that states this, what is the Constitution is doing is discriminate against women because it is telling us that we have some rights secluded to the women then we have human rights that have to be shared by the men as the head of the society. So that is one of my points.

Again it was not my intention to explain all this because we already have a right up about the Provincial Administration. Now, I would want you to clarify whether the intention of the government to abolish this or to restructure it because from your explanation and from my own understanding of the task is that it is being abolished. But it says that there will be elected councils. There will be a structure that will be coordinating this elective system so that we have a coordinated effort from the national to the lowest level. I seem not to understand that because the Constitution says, we are going to abolish but in your explanation, you said that we are going to have coordinating roles, I don't know where this comes from because it is not stated here.

**Kipkirui Arap Menjo:** Asante sana Madam Commissioner na watu wale ambao wako hapa siku ya leo. Jina ni Kipkirui arap Menjo. Langu ni kuhusu ile idadi ya wale watakuwa nominated from the constituencies waende Parliament. Tumeona idadi ya wale watakuwa nominated watakuwa wengi sana na tayari kama mmefanya devolution of powers from the Central Government to the Local Authorities, sion haja ya wengi waende huko juu na kazi kubwa iko upande huu.

Naona wengi wataenda juu na kazi nyingi ambayo inatakiwa iko kwa Local Authority ambapo kuna shida vile imetajwa pengine mmesikia kwamba ingekuwa bora kuwe na watu ambao ni technocrats wasaidie Local Authority to strengthen the work ambayo inatakiwa kuliko waende huko juu to duplicate the roles of the MPs sababu kama tayari MPs wameingia huko hakuna haja ya kuwa na wengine naona idadi nyingi, watachukua pesa nyingi ya serikali tena na tunajaribu ku-reduce ile gharama na expenses ya watu ambao wanajaa huko na hakuna kazi wanafanya.

Tena njia ya kuchagua mtu moja kwa district mimi naona hapo italeta kazi ambayo itafanya watu kutojua wanachagua mtu wa aina gani ita eneza corruption. Bado lazima mtu alete fedha akizunguka area hiyo yote na unapata anaingia tena hapo. Lets find a way kama ni Councillor amechaguliwa tuone huyo Councillor kazi yake ni namna gani afanyi kazi yake vizuri kwa sababu from the entire district, I am worried we are going back to the same track.

Pengine ningependa tu nipongeze Tume hili kwa kazi mzuri ambayo imefanya kukusanya maoni ya wananchi na mimi nashangaa kwa nini wale walikuwa wanafika juu wale wa Judiciary. I mean the legal profession na ninaona kazi yao imetengenezwa vizuri hata kuraisisha kazi zao. Kwa sababu mara nyingi wakienda kotini halafu mtu amepewa 'chai' aweze kushinda kesi kwa sababu ya ukora ambayo imefanyika na yeye ni lawyer mzuri alifanya kazi mzuri lakini sababu ya mambo vile inaenda mrama, his credibility is eroded lakini vile mambo imetengenezwa na vile imekuwa hapa, mimi naona hii proposal is good for everybody hata lawyers wenyewe wanatoa mhuri na client sasa hatakuwa akirushwa upande huu na upande ule kwa sababu mara wanawaambia hebu ongea na Judge vizuri, hebu ongea na lawyer vizuri. Hii imekuwa shida, kwa hayo machache naona mambo yote yangu vile inawezekana.

**Professor Tirop:** Mimi kwa majina naitwa Professor Tirop (*Laughter*) mimi ni mkaaji wa Eldoret hapa hapa, I do business. Kwanza nashukuru nawapa pongezi wale vijana wangu ambao walishugulika kwa mambo haya yote ya kukusanya habari kutoka Kenya nzima, kutoka kona mpaka kona. Kwa hivyo nawashukuru, nawapongeza pamoja na mama, kwa sababu wewe ni mama umefanya kazi mzuri sana.

Wananchi wangu au wanafunzi wangu, hii kazi yenu hii wengi walifikiri ni kazi kidogo sana hata hivyo wengine walioko nyumbani huko Eldoret lakini labda kama ingekuwa Mungu hangekua mbele yako au ya hawa hawangeweza kutoboa. Nikiongea namna hiyo, mimi naongea juu yangu, kuna swali mimi nataka kuuliza. (*Laughter*)

Jinsi mimi nataka kuuliza hawa watoto wangu, kama vile mimi ni mzee, sisi wazee kutoka sehemu mbali mbali tumekuwa na mambo moja hapa, ile tumeona. Vijana wetu wanakuwa na shida sana, mmesema nini juu ya vijana wetu, hii imekuwa ni shida sana. Anaoa bibi leo na kuja na bibi ndani ya nyumba kwa wiki moja kesho unasikia huyo kijana hana bibi, mmesema nini juu ya hiyo. Kwa sababu hiyo ni shida kubwa sana. Kwa sababu mimi ninafurahi, tunafurahi na mama, tunafikiri kijana yetu amepata bibi na baadaye unasikia yule alikuwa na Mmalaya tu sasa itakuwaje bibi na ni malaya. Mlisema nini juu ya hiyo sheria, lazima kuwe na sheria ya kulinda huyo mtoto wa mwenyewe. Lazima kuwe na sheria ambayo inalinda hii ya kuoa

asubuhi na jioni hana bibi. Lazima hiyo kitu ya muhimu ya kulinda msichana na mtoto wa mwenyewe halafu hapana komboa komboa nyumba kama shetani.

Langu la pili nikimalizia, mmesemaji juu ya vijana wa vijiji kutoka vijana wanaume na wasichana mwenyewe hawana heshima na akina baba zoa, hawana heshima na mambo zoa, mlisema nini juu ya hiyo sheria.

La tatu, katika nchi ya Kenya kwa jumla mlisema nini juu ya sheria ya mavazi ya Kiafrika na mavazi ya kigeni na wakoloni mamboleo. Tumepata aibu, tumepata mavazi mengine ambayo yametuletea aibu hata tumekosa mahali pa kuinginza macho zetu, imefanya karibu tuanguke kwa shimo. Hii ni aibu kubwa kwa Mwafrika, mlisema nini juu ya hiyo.

Basi nafikiri vijana kama nyinyi vijana wanaume ndio mnapendelea hiyo mavazi basi nataka kuuliza mzee mwingine halafu ajue ni kitu gani tutawaambia. Lakini kwa hivyo ni aibu angalia msichana wangu huyu, amevaa ngua ambayo inametameta. (*Laughter*), mimi nikiwa baba ni nini sijui juu ya huyu mtoto sababu mimi ndio nilimzaa. Si nilimzaa? Baba hajui nini, baba ni kipofu. Kwa hivyo hili ndio katika mila za Kiafrika lazima tupate mavazi ya kustahili mwanaume, msichana au mwanamke hata kama wageni wa kutoka nchi za mbali watasama this is for Kenyans. Hii ni aibu kubwa bwana. Kila siku tunakosana na Wasomali hapa kwetu juu ya mavazi lakini mavazi zingine nusu nusu ni fupi ni mavazi gani?

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Mzee.

**Christopher Odida:** Asante sana Bi Commissioner. Kwa majina mimi Christopher Odida. I want to ask a question in relation to fundamental rights of a Kenyan. Kenyans have had a problem which arise from poor planning and governance, for example you find that young Kenyans who are capable are not potentially exploited, that is I mean when you find someone goes to school and reach the current level defined by the government under its policy and then he or she ends up back at home. I think it is high time the Constitution state how these people's potentiality are going to be achieved. The Constitution should protect and should nature the achievement of the potentiality of Kenyans, this one I am asking whether the draft has in another defination or in another way, have talked of how the Kenyans especially young ones are going to mandated if not a social welfare then compulsory way of achieving income after striving and achieve the high maximum level of education. I would like to know whether it has give provision for that.

**Com. Salome Muigai:** I think that was the tenth one.

**Gilbert Bor:** No, this is the tenth one.

**Joseph Musinga:** My names are Joseph Musinga and actually my worry is implementation of public interest infact there is confusion in the draft. In fact I want to know the provision in the draft and the moderation in the councils from the village, to the

provincial Councils. For instance in Parliament requires moderation by the Speaker whether they decided to moderate the debate and come up with other goals or achieve goals but in what we have seen is not clear. I don't see that moderation, so I want to know the provision on that because even if it is to contribute to what the act says from the to the national level. Thank you.

**Com. Salome Muigai:** Thank you very much for your questions it show a lot of people are listening very carefully. I would like also to say that after this I will take 5 more questions and I would like to close this issue because the whole idea about this issue is not to hold the debate here, we could never do that. The whole idea is to introduce, to launch the draft and then you go out and create other avenues to allow those who get to debate. So even in my reaction to the question, I will deal with the questions that are asking for points of clarification and not the other things that we may not be able to address in detail.

The first question from David Omolo actually it is related to the last one, it is about the question of the governance at the local level and most of these will be done by the Parliament. But as far as is possible that is why we were not rigid. Hatukuwa tukitaka kusema ile serikali ya kata ama ya kijiji lazima ifanane kabisa kabisa na ile ye Bunge lakini maajirio yake, they are the same kuwa kutakuwa na coordinator ama tutakuwa na mshirikisha mwenye ni independent sio kunungunika mwenye ataweza kuita hiyo mkutano. Ama chama kikipatikana kilitengenezwa ilo baraza itengeneza ile sudi itachagua maofisa wake mwenye atakuwa akituita, mwenye atakuwa katiba, ndiye anaita mikutano na huyu ndio mwenye atakuwa mwenyekiti. Wengine wanafikiria kuwa na mwenyekiti wa kila mara na wengine watafikiria tutakuwa na wenye ofisi wa mzunguko kuwa atakuwa mwenyekiti kwa muda fulani lakini the module is still the parliamentary module ndio haitakubalisha the debate at all those levels.

Anauliza pia kama President atakuwa Mbunge, Rais hatakuwa Mbunge La.

